**[Toleo la Mei 2015]**

**Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia:**

**Kitabu cha Muongozo:**

**Kimetolewa na Kituo cha Ujamaa**

**Yaani *The Ujamaa Centre for Community Development & Research***

**(zamani kiliitwa *the Institute for the Study of the Bible & Worker Ministry Project*)**

**Sehemu ya 1**

**Yaliyomo**

Sura za Utangulizi

Sura ya 1: Utangulizi kuhusu Muongozo

Sura ya 2: Utangulizi kuhusu Kituo cha Ujamaa

Sura ya 3: Utangulizi kuhusu Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Sura ya 4: Wajibu wa Muwezeshaji

Sura ya 5: Wajibu wa Washiriki

Sura ya 6: Mfano wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Sura ya 7: Mfano wa namna ya kuandaa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Sura ya 8: Kueleza, Kumiliki na Kukuza theologia ya jamii:

Hitimisho kuhusu faida ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Sehemu ya 1

Sura ya 1

Utangulizi kuhusu Muongozo

Karibu kwenye Kitabu cha Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia! Yaliyomo katika Kitabu hiki ni matokeo ya kazi ya Zaidi ya miaka ishirini ya kuendesha Mtaala wa Biblia wa Mzingira Halisia. Ni mkusanyiko wa mafundisho ya mtaala wa Biblia toka kwa watumishi wa Kituo cha Ujamaa cha Maendeleo ya Jamii na Utafiti wa Kibiblia na Kitheologia, katika kitivo cha Dini na Falsafa, kwenye Chuo Kikuu cha KwaZulu-Natal, Afrika Kusini.

Katika Kituo cha Ujamaa, siyo tu kwamba tumeendesha Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa Zaidi ya miaka ishirini, bali pia tumetafakari Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa zaid ya miaka ishirini. Kwa hiyo, kitabu hiki ni matokeo ya duara la nadharia na vitendo – yaani ni matokeo ya kutafakari na kutenda. Kwetu sisi, Biblia ni raslimali ya mabadiliko ya jamii na mtu binafsi. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa namna nyingine ni mbinu ya kufundishia ambayo tumeitengeneza ili kuendesha mitaala yetu.

Tumeshafanya mamia ya mitaala ya Biblia katika mamia ya mazingira, ulimwenguni kote, na hasa miongoni mwa Wafrika weusi wa Afrika Kusini, walio maskini, tabaka la wafanyakazi, na waliosahaulika katika jamii. Watumishi wengi wa Kituo cha Ujamaa wanatoka katika jamii za namna hii.

Kwa kadri tunavyoendelea na mitaala hii, tumejitahidi kuelewa kile tunachokifanya, na kwa nini tunafanya hivyo, na kwa jinsi gani Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mbinu ya kufundishia yenye ufanisi. Mbinu ya kufundishia na kila mtaala uliyomo katika kitabu hiki ni matokeo ya kutenda na kutafakari. Kutafakari ndiko kumetuwezesha kusahihisha na kuboresha kile tunachokifanya na namna tunavyofanya; kutafakari pia kumetuongoza kujifunza kitu kipya, kuhusu mtaala husika na mbinu ya kufundishia tunayoitumia.

Kwenye ganda la kitabu kuna picha ambayo ni kazi ya Sanaa iliyotengenezwa kwa chuma toka Calcutta, India. Picha hiyo inawasilisha duara la kutenda na kutafakari. Umbo hilo la picha linaonekana kuganda mithili ya barafu katikati ya tukio la kutenda (upande wa kulia) na kutafakari (upande wa kushoto). Kazi na uchambuzi vinaonekana dhahiri na kwa uzuri katikati ya matukio hayo mawili. Umbo hili yamkini linawasilisha vizuri kazi ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

Kitabu hiki kitengenezwa kama **zana ya kufundishia**. Hii ina maana kwamba kimetengenezwa kwa lengo la kufundisha mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Njia pekee ya kujifunza Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni kwa vitendo! Kujifunza huja kwa njia ya kutenda. Kwa hiyo kitabu hiki kinakupa mitaala kadhaa ya Biblia ambayo tumeshaifanya, na imeandikwa kwa namna ambayo inawawezesha wengine kufanya mitaala hiyo. Pia unaweza kupata mitaala kadha wa kadha ya Biblia katika tovuti yetu http://ujamaa.ukzn.ac.za

Kitabu hiki siyo cha maswali na majibu. Mitaala ya Biblia na tafakari zake ni miongozo. Kila mtaala umeshapitia mchakato mrefu wa kutafakari na kusahihisha. Sisi tumejifunza kwa njia ya

kutenda, tungependa na wewe ufanye vivyo hivyo. Yafaa uone kwamba mitaala hii ni yako, na uwe na uhuru wa kuitumia utakavyo kwa uhuru kwa kuzingatia mazingira yako; na pia utengeneza mitaala mingine ambayo pia itajibu mahitaji ya mazingira yako. Kwa hiyo kuna umuhimu wa kuwa na uhuru katika kutumia mitaala hii.

Mbinu zilizotumika hapa zimezingatia ufahamu wetu wa mazingira yetu, na kadri unavyoendelea na kitabu hiki yafaa uamue ikiwa mbinu zilizotumika katika kitabu hiki zafaa katika mazingira yako au la. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mbinu ya kufundishia – ni njia ya kukuwezesha kutenda, na siyo kanuni fulani za hesabu.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mbinu inayofanana na mbinu nyingine za Mtaala wa Biblia ambazo matokeo ya ushirikiano kati ya wataalamu wa Biblia na theologia wanaojihusisha na jamii, wasomi wanamageuzi, na Wakristo wasomaji wa kawaida wa Biblia (wanaojua kusoma na wasiojua). Wengi yamkini mnafahamu mbinu ya usomaji wa Biblia itwayo Tazama-Amua-Tenda, ambapo mchakato wa usomaji wa Biblia huanza na uchambuzi wa mazingira halisia ya maisha (Tazama), na kisha Biblia husomwa tena ili kuwezesha andiko kunena na mazingira husika (amua), kisha tena mchakato huendelea na hatua ya kutenda kwa kadri tunavyoitikia lile ambalo Mungu anasema nasi (Tenda). Uchambuzi wa maisha ya jamii hutuwezesha kuelewa maisha yetu halisia; kuisoma Biblia tena na tena hutuwezesha kuamua ikiwa maisha yetu halisi yako vile ambavyo Mungu anakusudia yawe; na mpango wa kutenda hutuwezesha kutenda kazi pamoja na Mungu ili kubadilisha maisha yetu. Mchakato huu ni endelevu, hujirudiarudia, kwa kuwa kila tendo moja hutuongoza katika kutafakari (Tazama), na kadhalika. Hili ni duara la kutenda na kutafakari.

CEBI (ni kutuo cha mtaala ya Biblia kama yetu, kiko Brazil) kinatupa faida ya mambo mawili katika mchakato wa duara la theologia ya vitendo. Mchakato wao una vipengere vya Tazama-Amua-Tenda-Sherekea-Tathmini. Baada ya kutenda, kundi husherekea kile walichofaulu kufanya katika jamii, hufanya hivyo kiliturgia na kijamii. Na baada ya sherehe hufuata tathmini. Kundi hutathmini mchakato mpaka walipofikia, na kisha huendelea kuweka mpango wa kazi inayoendelea.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mojawapo ya mfumo wa kanuni ya Tazama-Amua-Tenda. Kwanza, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huzingatia uchambuzi yakinifu na mahitaji ya jamii husika ya maskini, tabaka la wafanyakazi, na wanyonge. Mtazamo wao wa maisha halisia ndiyo msingi wa mtaala wote wa Biblia. Pili, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unatoa fursa ya kufanya uchambuzi yakinifu wa kitheologia, kutuwezesha "kusoma ishara za nyakati". Biblia husomwa kwa uangalifu na kwa ukaribu sana ili kusikia sauti maalumu katika maandiko ya Biblia na katika mazingira yake ya kihistoria na kijamii, na kutuwezesha kupata zana za kitheologia za kutuwezesha kutafakari na kufanya uchambuzi yakinifu wa jamii. Na tatu, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huhitimishwa kwa kutumia zana na raslimali za kitheologia kwa ajili ya kupanga mabadiliko ya mtu binafsi na ya jamii.

Kitabu hiki kimeandaliwa ili kukuwezesha kufuatisha kwa vitendo mbinu ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Kitabu hiki kimeandaliwa ili kuongeza na kukamilisha mambo yanayopungua katika vitabu vifuatavyo:

• West, Gerald. *Contextual Bible Study* (Pietermaritzburg: Cluster Publications, 1993) [tafsiri ya kichwa cha kitabu, 'Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia']

• West, Gerald. *The Academy of the Poor: Towards a Dialogical Reading of the Bible* (Pietermaritzburg: Cluster Publications, 2003) http://clusterpublications.co.za [tafsiri ya kichwa cha kitabu, 'Taaluma ya Maskini: Mwelekeo wa Kusoma Biblia kwa Majadiliano']

• Kitabu kingine kinachohusiana sana na vilivyoorodheshwa hapo juu ni: Riches, John, Helen Ball, Roy Henderson, Craig Lancaster, Leslie Milton, and Maureen Russell. *What Is Contextual Bible Study? A Practical Guide with Group Studies for Advent and Lent*. London: SPCK, 2010. [tafsiri ya kitabu, 'Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni nini? Muongozo wa Vitendo kwa Vikundi vya Mtaala wakati wa Majilio na Kwaresma]

• Kazi ya Kituo cha Ujamaa inatokana na uhusiano wa miaka mingi na shirika la CEBI la Brazil (tazama hapo chini), kitabu kifuatacho ni miongoni mwa vitabu ambavyo tumenufaika navyo sana: Dreher, Carlos A. *The Walk to Emmaus*. São Leopoldo: Centro de Estudos Bíblicos, 2004. [tafsiri ya kitabu, 'Safari ya Emau']

• Schinelo, Edmilson, ed. *The Bible and Popular Education*; *Encounters of Solidarity and Dialogue*. São Leopoldo: CEBI, 2009. [tafsiri ya vitabu, 'Biblia na Elimu kwa Wote'; 'Kukutana na Mshikamano na Majadiliano']

Mitaala imepangwa hatua kwa hatua. 'Hatua' ni miongozo ili kukuwezesha kuuzoea mchakato. Mara ukishauzoea mchakato wa mtaala, unaweza kuandaa mtaala wako mwenyewe, na unaokufaa.

Kuna njia mbalimbali za kutumia kitabu hiki. Wengine wanaweza kutumia kitabu hiki kwa mtiririko wake maalumu, kwa kufuata kila mtaala, mmoja baada ya mwingine, hadi mwisho. Wengine wanaweza kutumia sehemu ya kwanza ya kitabu hiki, na kisha kuchagua mtaala fulani wa Biblia ambao unahusiana na mazingira yao.

Ni vema ifahamike kwamba ingawa mitaala hii iliandikwa kwa Kiingereza kwa mara ya kwanza, mitaala hii pia imeendeshwa kwa lugha nyingine za Kiafrika. Una uhuru wa kutafsirika katika lugha yoyote ambayo utaitumia kuongozea mitaala.

Kila Mtaala wa Biblia katika kitabu hiki una vipengere kadha wa kadha. Kipengere cha msingi ni maswali ya Mtaala wa Biblia. Maswali ndiyo 'mifupa' ya Mtaala wa Biblia. Kadri unavyotumia maswali katika kikundi, kikundi hicho kitaongeza 'nyama' katika mifupa hiyo, na mifupa hiyo itaishi (Ezekieli 37)!

Pamoja na kipengere hicho cha msingi, katika baadhi ya mitaala ya Biblia kuna kutafakari mtaala wa Biblia kwa kuzingatia uzoefu wa maisha. Kipengere hiki ni muhimu katika kukusaidia kuelewa jinsi kikundi kinavyoyashughulikia maswali. Kikundi chako kinaweza kujibu tofauti! Kipengere hiki kinaitwa: "Hitimisho la Mchakato wa Usomaji katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia."

Hatimaye, katika baadhi ya mitaala ya Biblia kuna kipengere ambapo huwa tunatafakari mbinu ya Mtaala wa Biblia.  Kipengere hiki kimewekwa kwa ajili ya wale wanaotaka kuchimba Zaidi katika mchakato wa Mtaala wa Mazingira Halisia.  Kipengere hiki kinaitwa "Mbinu ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia."

Mitaala katika kitabu hiki ni kwa ajili ya mtu yeyote anayependa kuitumia.  Muwezeshaji wa Mitaala ya Mazingira Halisia siyo lazima awe amesomea theologia. Siyo lazima awe kasisi, au mhudumu wa kanisa.  Mitaala hii ya Biblia ni kwa ajili ya mtu yeyote anayetaka kusoma na kuelewa uzoefu wake wa maisha na mazingira yake kwa kutumia Biblia.  Mitaala imeandaliwa katika namna ambayo inaweza kumfaa mtu yeyote anayetamani mabadiliko katika jamii kwa njia ya usomaji wa maandiko.

Kitabu hiki pia ni mwito kwa watheologia na wataalamu wa Biblia wanaojihusisha na mambo ya kijamii kujitoa wenyewe na kutoa raslimali zao kwa ajili ya jamii zilizosahaulika; pia ni mwito kwa wasomaji wa kawaida wa Biblia kutumia nyenzo zilizopo za kitheologia ili kuwawezesha katika usomaji wa kina wa Biblia.

## Sura ya 2

## Kuhusu Kituo cha Ujamaa

Kituo cha Ujamaa ni taasisi inayounganisha mitaala ya biblia katika taasisi za kitaaluma na wasomaji wa Biblia wa kawaida wa Afrika (wanaojua kusoma na wasiojua) katika jamii za waumini. Watumishi wa Kituo cha Ujamaa kwa sehemu kubwa ni 'wanazuoni wanaojihusisha na mambo ya jamii', na wao wenyewe wanatoka katika jamii maskini, tabaka la wafanyakazi, na jamii zilizosahaulika.

Mitaala yote ya Biblia katika Kitabu hiki cha muongozo inatoka katika hali ya 'maisha halisi' na mazingira halisia ya jamii. Mitaala 'imeandaliwa' kwa kipindi kirefu, kwa kuhusisha watu wengi na makundi kadha wa kadha ya watu. Kwa hakika, kinachotokea ni kwamba Kituo cha Ujamaa hualikwa na vikundi katika jamii ambavyo huomba wana Ujamaa kushiriki pamoja nao katika Mtaala wa Biblia au kutakafari Biblia. Watumishi wa Ujamaa wanapoalikwa kwanza huuliza ikiwa mwaliko unatoka kwenye kikundi ambacho kina mfumo maalumu. Vikundi vyenye mfumo maalumu wa uongozi huwa vina hali ya kujitambua zaidi kuliko vikundi visivyo na uongozi. Ni hali hii ya kujitambua ndiyo inayofanya kikundi kione kuwa shughuli ya mtaala wa Biblia ni yao na ya kwamba kikundi ndicho kimealika Kituo cha Ujamaa kushiriki, na pia kikundi ndicho 'hutoa mrejesho' kwa Kituo cha Ujamaa. Kwa namna fulani kushiriki katika makanisa au kukundi cha jamii hufunua na kudhihirisha mifumo ya mamlaka iliyofichika. Kwa hiyo, Kituo cha Ujamaa hupenda kushirikiana na vikundi ambavyo havitishiki na uwepo wa watumishi wa Kituo cha Ujamaa na zana zake za kitaalam; vikundi ambavyo vinajua lengo lao na kitu gani wanahitaji kutoka katika ushirikiano katika mtaala wa Biblia; vikundi ambavyo vinajua vitakuwa na mchango wake pekee katika mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Dhamira kuu ya Kituo cha Ujamaa ni kufanya kazi katika mazingira halisia ya kikundi husika, kwa kuzingatia uzoefu na ufahamu wa kikundi chenyewe.

Kama mwaliko wa kufanya mtaala wa Biblia unatoka kwenye kikundi ambacho hakina mfumo rasmi, au kikundi hakielewi lengo lake katika mtaala wa Biblia, basi Kituo cha Ujamaa hutoa muongozo utakao kiwezesha kikundi kuwa na mfumo rasmi au kulipambanua lengo lake katika kutaka kuwa na mtaala wa Biblia. Ni muhimu sana kwa kikundi chenyewe kufanya uchambuzi yakinifu wa mazingira yake (yaani hatua ya *Tazama*). Kituo cha Ujamaa pia huvitia moyo vikundi vyenye lengo moja katika jamii na kanisa kuungana. Kwa mfano, Kituo cha Ujamaa kinaweza kushauri kikundi cha akinamama cha Anglikana kualika vikundi vingine vya akinamama kutoka katika eneo lao ili kuunda kikundi kinachounganisha madhehebu mbalimbali ili kuwa na mtaala wa Biblia mmoja.

Mchango wa Kituo cha Ujamaa ni kuwezesha warsha ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Warsha huzingatia mada au jambo linalotokana na kikundi chenyewe. Kwa mfano, kikundi kinaweza kuamua kushughulikia suala la ukatili dhidi ya wanawake, au uongozi, au ukosefu wa ajira, au VVU na UKIMWI. Mara nyingi warsha huwa pia zinajadili na mambo mengine pia na zana mbalimbali; Mtaala wa Biblia huzingatia yote yanayojitokeza ili kuleta mchango katika jamii. Kuna zana nyingi za mabadiliko ya mtu binafsi na jamii; Mtaala wa Biblia ni zana

mojawapo ya mabadiliko; hata hivyo zana muhimu ni jamii zenyewe ambamo Biblia ni andiko muhimu.

Katika uchambuzi yakinifu wa jamii, Kituo cha Ujamaa kinatambua kuwa watu binafsi na mifumo ya jamii inahitaji mabadiliko. Kanisa mara nyingi limesisitiza mabadiliko ya mtu binafsi, lakini Biblia ina mengi ya kutuambia kuhusu uovu na mifumo mibovu na ya kwamba kuna haja ya kuibadilisha mifumo hiyo. Mitaala ya Biblia ya Mazingira Halisia hushughulika na mtu binafsi pamoja na mifumo ya jamii.

Kila mtaala wa Biblia katika kitabu hiki cha muongozo umefanya na kikundi halisi katika mazingira halisi. Kila kikundi kimechangia uzoefu wake, mahitaji yake, ufahamu wake na raslimali zake katika mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Vivyo hivyo, wewe na washiriki wako katika kikundi mnahimizwa kuifanya mitaala hii kuwa ni yenu pia, na kuitumia katika namna inayoendana na uzoefu wenu, ufahamu wenu na mazingira yenu.

Kituo cha Ujamaa kinafanya kazi nadharia ya makusudi sita (kusudi moja ni sawa na kidole kimoja katika mkono mmoja, halafu ongeza na kidole kingine katika mkono mwingine!). Haya ndiyo makusudi sita ya Mtaala wa Biblia; kwa maneno mengine, haya ndiyo mambo sita tunayoyathamini katika uendeshaji wetu wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia (MBMH):

1. Jamii, Jamii ndiyo mwanzo na lengo la Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia (MBMH); jamii ndiyo vazi la MBMH; jamii za maskini waliohamasika, tabaka la wafanyakazi, na makundi ya wanyonge ndiyo hatua ya msingi na uhalisia wa msingi wa MBMH; Jamii pia ndiyo lengo kuu la MBMH, kwa kuwa MBMH inachangia kuleta ukombozi katika jamii, utu kamili na uzima tele kwa wote.

2. Yakinifu, MBMH huwezesha uchambuzi 'yakinifu' wa nyanja zote za maisha; hasa, MBMH inayakinisha na kufanya uchambuzi wa mtu binafsi, jamii na maandiko ya Biblia, kwa kutumia maswali maalumu na yenye mpangilio, na kwa namna hiyo huandaa mazingira ya kimdahalo kati ya mtazamo makini wa maisha na usomaji yakinifu wa Biblia.

3. Ushirikiano, MBMH hufanyika katika mazingira ya ushirikiano katika kazi ya jamii na ushirikiano katika ufafanuzi wa Biblia miongoni mwa jamii maskini zilizohamasika, tabaka la wafanyakazi, na wanyonge, na pia wanataaluma watakaomageuzi, na wataalamu wa Biblia na theologia wapenda mabadiliko ya jamii na wanaojihusisha na maisha ya jamii; Ushirikiano huanza na kazi halisi katika mapambano ya maisha halisia; kisha Ushirikiano huendelea na kuhusisha ushirikiano katika kufafanua Biblia na kushiriki pamoja katika 'kuitenda' theologia, kuondoka kwenye theologia iliyozoeleka na kuelekea kwenye theologia ya watu na theologia ya kiunabii.

4. Mabadiliko, MBMH hutumia Biblia kama zana na kujenga hoja kwa ajili ya kazi ya kuleta mabadiliko katika jamii; Mabadiliko huhusisha mtu binafsi na jamii, pamoja na kanisa (na dini zote kwa ujumla); lengo kuu la mabadiliko ni kubadilisha muundo na mfumo wa jamii, na njia kuu ya mabadiliko ni geuza itikadi na fikra za kitheologia.

5. Mazingira, MBMH hujikita katika nyanja nyingi za mazingira halisi ya maisha, na hasa nyanja za mifumo na miundo ya maisha halisia; MBMH inatambua kuwa mtu binafsi, jamii, na

maandiko ni matokeo ya nyanja hizi za maisha halisia; kipekee, MBMH ni zana inayowezesha kuchambua nyanja za mazingira ya kiuchumi, kisiasa, na kidini; MBMH hutambua kuwa mazingira ya maisha hubadilika.

6. Mapambano, katika MBMH ‘mapambano’ ni dhana ya msingi kijamii na kitheologia; katika MBMH tunatambua kuwa mapambano ni sehemu ya mazingira ya maisha halisia, na kwa hiyo katika MBMH tumechagua kusimama upande wa Mungu wa uzima dhidi ya miungu wa mauti; kwenye MBMH ‘uwanja’ mkuu wa mapambano ni itikadi na theologia; MBMH inatambua utata uliyopo katika usomaji wa biblia yenyewe, ikiwa ni pamoja na theologia za kibiblia zinazoleta uzima na theologia za kibiblia zinazoleta mauti; MBMH ‘hugombana’ na maandiko ya biblia ili kuleta uzima.

Mahali popote ambapo Biblia inakubalika kama andiko muhimu tena takatifu, basi mahali hapo Mtaala wa Biblia unaweza kuwa chombo kinachofaa kama zana ya kidini ya kuleta mabadiliko ya jamii. Mtaala wa Biblia peke yake hauwezi kutatua matatizo yetu, bali unaweza kuweka mazingira ya utakatifu yaliyosalama ya kutuwezesha kushughulikia mambo magumu; pia mtaala unaweza kutupa zana za ziada za kupambana na mambo yanayotukabili katika mazingira yetu. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unasisitiza kuichambua mifumo ya maisha yetu sasa, na maisha katika zama za biblia, na kuyaleta maisha haya yote pamoja katika kioo cha tathmini kupitia Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

## Sura ya 3

## Kuhusu Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Mambo mengi yaliyomo ndani ya sura hii utayaelewa zaidi mara ukishiriki katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, au ukiongoza mtaala mmoja. Hata hivyo itakufaa zaidi kuusoma utangulizi huu wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Hakika, unahimizwa kwa kweli kusoma sehemu hii yote kabla hujaanza kutumia mtaala wowote katika kitabu hiki cha muongozo.

Kuna **hatua tano** zinazoweza kuainishwa katika kuandaa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Ifahamike kuwa 'hatua' hizi zinatoa muongozo tu siyo kanuni.

### Hatua ya 1 – Ainisha Mada (Tazama)

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa kawaida huanza na mambo yahusuyo maisha halisia ya jamii husika. Mara zote mtaala huongozwa na **mada** au masuala ambayo jamii inashughulika nayo. vikundi vya mtaala ambavyo vina mfumo wa uongozi huwa vinatambua kwa dhahiri kabisa masuala yanayoikabili jamii yao.

Hata hivyo, vikundi vipya vya mtaala, vinahitaji kuwezeshwa ili kukutana na kufanya uchambuzi yakinifu wa mazingira ya jamaii. Hii ni hatua muhimu ya kwanza! Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa kawaida huanza na mada au masuala halisi yanayoihusu jamii.

> Maelezo kwa mtumiaji wa muongozo huu kuhusu kuainisha mada
>
> Kila mtaala katika muongozo huu una mada. Baadhi ya mitaala inaweza kutumika kuzungumzia mada zaidi ya moja. Unapochagua mtaala wa kutumia, yafaa uchague mtaala ambao una mada inayofaa kwa mazingira ya kikundi chako. Kwa kweli, ni jambo zuri kuwa na orodha ya mada ili kikundi kiitafakari na kuamua mada gani inagusa zaidi na inahusu jamii yao zaidi. Ukurasa wa 'Yaliyomo' una orodha ambayo inaweza kutumika wakati kikundi kinapowaza mada gani kiitumie.

### Hatua ya 2 – Kubainisha Kifungu cha Biblia (Amua)

Mara baada ya kuchagua mada, kazi ya kuupanga mtaala wa Biblia inaweza kuanza. Baada ya kupata mada sasa yafaa kubainisha kifungu cha Biblia kinachoendana na mada – kifungu kitakacho 'ieleza' mada.

Kituo cha Ujamaa kinatumia njia mbili. Ingawa tunaweza kusoma vifungu vya Biblia ambavyo ni chaguo la kikundi, pia tunaweza kuwaonyesha vifungu ambavyo hawajavizoea. Kwa maneno mengine, tunasoma vifungu tulivyovizoea kwa njia tusizozizoea (kwa kuvitazama kwa njia tofauti), na pia tunasoma vifungu tusivyovizoea (vifungu vinavyoachwa, vinavyokwepwa, na vilivyosahaulika na kanisa). Kusoma vifungu vilivyozoeleka kwa njia zisizozoeleka, na kusoma vifungu visivyozoeleka kunawezesha washiriki wa kikundi cha mtaala wa Biblia kuisoma Biblia kwa upya, na kuisikia Biblia ikinena kwa njia mpya.

Kwa kuhusianisha kifungu cha Biblia na mada fulani, mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unaweza kuibua **vipengere vyenye uhusiano** kati ya mazingira yetu na mazingira ya zama za Biblia. Mara zote siyo rahisi kubainisha kifungu kinachofaa. Kwa hiyo kuna umuhimu wa kuwa msomaji wa Biblia 'wa maisha', kwa kujituma wenyewe kuisoma Biblia kwa upana na kina chake chote.

Maelezo kwa mtumiaji wa muongozo huu kuhusu kutafuta kifungu

Vifungu vya maandiko kwa ajili ya muongozo huu vimekwisha chaguliwa wakati wa kuandaa mitaala. Wewe na washiriki wa kikundi chako yafaa muwe huru kuufanya mtaala huu kuwa ni wenu kwa njia ya kuchunguza vifungu vya maandiko na hata kuongeza vingine vinavyofaa kwa mada mliyochagua. Hata hivyo, ni muhimu kutafakari kifungu kimoja kwa wakati mmoja. Sharti muepuke tabia ya kurukaruka toka kifungu kimoja hadi kingine. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia umeundwa kuwasaidia kusikia sauti ya kifungu kimoja kwa kina zaidi kwa wakati mmoja.

Hatua ya 3 – Kuandaa Maswali (Kuchambua na Kuhusianisha Kifungu na Mazingira)

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia msingi wake ni kujiuliza maswali kuhusu mazingira yetu na kifungu cha Biblia. Kwa hiyo, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unatumia aina mbili ya maswali.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huanza na huishia na maswali yahusuyo mazingira halisia ya maisha ambayo hutupa muundo wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Mawali haya yahusuyo mazingira huitwa 'maswali ya kujitambua kama jamii', kwa sababu yanatokana na uzoefu wa jamii na raslimali zake. Ni maswali yanayotokana na uzoefu wa maisha na ufahamu wa kitheologia wa washiriki wenyewe. Ni maswali yanayotokana na aina ya ufafanuzi wa maandiko ambao jamii imeshausikia katika makanisa.

Kutokana na muundo huu wa maswali yahusuyo jamii, kwa uangalifu tunaandaa maswali yahusuyo kifungu cha maandiko, ambayo yanakiwezesha kikundi kutafakari kifungu cha maandiko kwa utaratibu. Maswali haya yahusuyo kifungu cha maandiko pia huitwa 'maswali ya kujitambua kwa dhati kifikra', kwa sababu yanatokana na zana zenye mpangilio na muundo maalumu wa utaalamu wa kibiblia.

Changamoto kwa wataalamu wa Biblia wanaojihusisha na mabadiliko ya jamii ni kuandaa maswali yanayofungua mwanya wa kujadili kifungu cha maandiko katika namna ambayo inagusa mazingira halisia ya washiriki.

Zana za utaalamu wa kibiblia huzingatia aina tatu za mazingira ya kifungu cha maandiko:

- *Nyuma* ya kifungu (huzingatia historia na maisha ya jamii husika kifungu kilipoandikwa);
- *Juu* ya kifungu (huzingatia kifungu chenyewe, muundo wa sarufi na fasihi yake); na
- *Mbele* ya kifungu (huzingatia taswira za maisha ya ulimwengu ambayo kifungu husika kinaposomwa kinaweza kuyaangazia kwa msomaji wa kifungu wa zama hizi).

Aina mojawapo kati ya aina hizo tatu za mazingira ya kifungu cha maandiko inaweza kutumika katika mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Tumeandaa mbinu, kwa maneno mengine njia maalum, ambayo kwa kawaida tunaitumia tunaposhughulika na aina hizo tatu za mazingira ya kifungu cha maandiko:

1. Tunaanza na mazingira yaliyo mbele ya kifundu, kwa kupata mawazo ya washiriki kwa kuwauliza kifungu kinahusu nini. Hapa huwa wanaombwa kutumia ufahamu wao kueleza kifungu kina maana gani kwao, au wamewahi kukitafisiri vipi.

2. Kisha tunazingatia kifungu chenyewe, kwa kuruhusu kifungu 'kitoe sauti yake' kupitia sauti za washiriki. Hapa hutumika maswali ambayo huwafanya wasomaji wasome kifungu kwa ukaribu, polepole na kwa uangalifu.

3. Kisha tena, hutumika maswali yanayowaalika washiriki kuchunguza mazingira yaliyo nyuma ya kifungu cha maandiko. Kwa kawaida maswali ya aina hii huandaliwa kwa kulenga kifungu chenyewe (tazama maelezo ya hapo juu), la sivyo, muwezeshaji anaweza kutunga swali au maswali anayochunguza historia na maisha ya ulimwengu wakati kifungu husika cha maandiko kilipoandikwa.

4. Hatimaye, tunahitimisha kwa kuzingatia tena mazingira yaliyo mbele ya kifungu cha maandiko, kwa kuchunguza kifungu kinatueleza kitu gani katika wakati wetu wa sasa. Mpaka hapa tunakuwa tumeshasoma kifungu kwa kutumia zana 'za ndani' (juu ya kifungu) na 'za nje' (nyuma ya kifungu, sasa tunapaswa kujiuliza kwa mara nyingine tena kwamba kifungu kinatuambia nini sisi wa leo.

Maswali yahusuyo muundo wa sarufi na fasihi ya kifungu (kipengere cha 2 hapo juu), punguza kasi ya mchakato wa usomaji, ili kuwawezesha washiriki kusoma kifungu kwa uangalifu na makini zaidi kuliko usomaji wao wa kawaida. John Riches toka kikundi cha Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia cha Glasgow, Scotland, anazungumzia umuhimu wa kupunguza kasi ya mchakato wa usomaji, na ya kwamba hatua hii huwapa wasomaji muda zaidi wa kutafakari kifungu. Maswali yahusuyo sarufi na fasihi ya kifungu pia humuwezesha msomaji kuwa na taswira ya mazingira ya ulimwengu wa kifungu husika, na kumuwezesha msomaji kuhisi kana kwamba yumo ndani ya ulimwengu huo na kujiweka ndani ya ulimwengu huo. Msomaji yeyote anaweza kupata taswira ya namna hiyo, hata kama hajawahi kufanya mafunzo ya uchambuzi wa maandiko. Maswali ya mtaalam wa Biblia anayejihusisha na mabadiliko ya jamii huwapa washiriki fursa ya kukisoma kifungu kwa upya, na kubainisha mambo mbalimbali ya kina yahusuyo kifungu cha maandiko. Kwa kuzingatia mambo ya kina ya kifungu, washiriki wengi sasa watapenda kujua zaidi kuhusu mazingira ya ulimwengu ambamo kifungu kilipoandikwa. Huu ndiyo wakati wa kutumia maswali yahusuyo historia na maisha ya ulimwengu wa Biblia, ambayo hutupa fursa ya kurudi nyuma kabisa katika zama za kale na kuingia katika ulimwengu ambao maandiko ya Biblia yalitokea.

Kwa ufupi, baada ya kusoma kifungu tena na tena, pia kusikia sauti ya maneno ya kifungu kwa kina, na kusikia sauti ya maneno ya kifungu katika ulimwengu wake, sasa tunaweza kujiuliza

tena kifungu kinatuambia nini na jinsi gani tunaweza kuitikia sauti yake na kutenda. Mchakato huu huwezesha kifungu cha Biblia kuwa na sauti ya wazi na ya pekee katikati yetu; sauti zetu huungana pamoja na sauti za maneno ya kifungu ili kumsikia Mungu akisema nasi toka katika ulimwengu uliyompya kwetu; kisha tunajitoa kwa Mungu na kwa ajili yetu wenyewe katika mpango kazi.

Ni muungano huu wa maswali yahusuyo mazingira yetu na yale yahusuyo kifungu cha maandiko ndiyo unaounda mbinu ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Kuwa kujiuliza maswali yahusuyo kujitambua kwa jamii na kujitambua kwa dhati kifikra kuhusu ufahamu wa maandiko, kifungu cha maandiko husema nasi kwa namna mpya katika maisha yetu halisi. Mchoro wa MBMH, mithili ya silesi mbili za mkate na nyama katikati yake, unatupa kielelezo cha jukwa la ushirikiano kati ya zana za jamii na za kitaaluma, pia uhusiano kati ya jamii na dhana ya kujitambua kwa dhati kifikra kupitia zana za kitaalam za uchambuzi wa maandiko. Yafaa ifahamike kuwa mchakato wa 'ku-Tazama' huanza kabla ya mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia haujaanza rasmi, kwa kuwa mada ya Mtaala wa Biblia hutokana na uchambuzi yakinifu wa jamii ambamo Mtaala wa Biblia unafanyika. Vilevile, mchakato wa 'Tenda' huendelea kwa muda mrefu hata baada ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kukamilika, kwa kuwa hatua ya mpango kazi huwa ni mpango kazi wa jamii husika na hivyo mpango huo hutegemea raslimali na muda muafaka wa utekelezaji wa jamii husika.

Mchoro wa MBMH

'silesi mbili za mkate na nyama'

| | | |
|---|---|---|
| Mkate | Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia Huanza na Uhalisia, uzoefu, raslimali na zana za jamii | TAZAMA |
| Nyama/Jamu | Katikati Tunasoma Biblia tena na tena, polepole, kwa uangalifu na ukaribu, Tukitumia zana za utaalamu wa Biblia | AMUA |
| Mkate | … na huishia na Uhalisia, uzoefu, raslimali, na zana za jamii | TENDA |

**Hatua ya 4 – Kutanabaisha na Kumiliki (Kuuweka bayana na Kujimilikisha Mtaala wa Biblia)**

Mara maswali yanapokamilika, sasa maisha ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia yanakuwa yameanza! Kuanzia hatua hii, kinachojitokeza kwenye mtaala ni matokeo ya kazi ya

kikundi husika.  Mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia una nguvu ya kuwawezesha washiriki kuweka bayana na kumiliki ufafanuzi wao wa kifungu fulani cha maandiko kwa kuzingatia mazingira yao. Kuunganisha maswali yahusuyo mazingira halisia na kifungu cha maandiko kuna uwezo wa kubainisha uhusiano uliyopo kati ya kifungu cha Biblia na theologia ya mazingira halisi ya washiriki.  Uhusiano huu kati ya kifungu cha maandiko na mazingira halisi mara nyingi huwapa washiriki uwezo zaidi wa kuweka bayana ufahamu wao halisi wa kitheologia unaojitokeza, hata ufahamu ambao wanaweza kuwa nao lakini bado hauko wazi kwao.

Ikiwa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia utakuwa mahali salama kwa washiriki – mahali pakutegemewa na panapokubalika – basi washiriki wanaweza kuanza kuonyesha wazi theologia halisi.  Theologia halisi ni theologia ambayo imeumbika ndani ya mtu mwenyewe, kwa sababu ya urithi wa kitheologia, na pia uzoefu wa mtu na Mungu wake na ulimwengu anaoishi.  Kwa watu wengi waliosahaulika katika jamii, theologia zao halisi huwa tofauti na theologia za kanisa; kwa hiyo, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisi ni zana muhimu ya kuwezesha makundi yaliyosahaulika katika jamii ili kupaza sauti zao na kueleza wazi theologia zao halisi.  Mara nyingi, washiriki kutoka katika mazingira yaliyosahaulika wana fursa ndogo ya kuwashirikisha wengine theologia yao halisi (yaani imani na ufahamu wao halisi kuhusu Mungu na ulimwengu). Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia hutoa fursa kwa washiriki kuiweka bayana na kuimiliki theologia yao halisi katika mazingira yao husika.

Katika maisha ya watu wengi wanaoshiriki katika makanisa, theologia zao halisi kwa kiasi fulani zinazungumzwa, zinakubalika, zinaelezwa na kutendwa katika mikusanyiko ya hapa na pale ya makanisa.  Kwa sababu hii, Wakristo wengi huenda kwenye kanisa moja ‘mchana’ na kwenye kanisa jingine wakati wa ‘usiku’.  Kwa kuwa wameumbwa kwa mfano wa Mungu, kuna hamu kubwa myoyoni mwao ya kusikia theologia yao halisi ikizungumzwa na kanisa.  Kwa bahati mbaya jambo hili linatokea mara chache sana, lakini mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisi unatoa fursa.

**Hatua ya 5 – Kuandaa Mpango Kazi (Tenda)**

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huishia na kutenda. Kila kikundi kidogo kinachoshiriki Mtaala wa Biblia lazima kiandae **mpango kazi**.  Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia haulengi kufafanua Biblia peke yake; bali ni njia ya kuruhusu Biblia kutuwezesha kuubadilisha ulimwengu wetu ili ufalme wa Mungu uje hapa duniani, kama ulivyo mbinguni!  Kwa sababu Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mchakato wa kuwawezesha washiriki kuiweka bayana na kuimiliki theologia yao halisi katika mazingira yao husika, mpaka hatua hii washiriki wanakuwa wameongezewa uwezo zaidi wa kutenda.  Kutenda ni matokeo ya lazima ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, ilimradi tu kikundi kina umiliki mchakato wa mtaala kuanzia mwanzo.  Vikundi kwa kawaida huwa vinaweza kujua kile kinachowezekana na kisichowezekana kufanyika katika jamii yao husika.  Pengine inaweza isiwe busara kutekeleza mpango fulani kwa sababu ya vipingamizi vya mazingira husika, lakini yamkini mpango wa aina nyingine unaweza kutekelezeka katika mazingira hayo.

Kituo cha Ujamaa huwahimiza washiriki kuandaa mpango kazi katika hatua tatu: kwanza, andaa mpango unaowezakutekelezeka pasipo mahitaji ya ziada ya raslimali; pili, andaa mpango unaowezakutekelezeka kwa kutumia mahitaji ya ziada ya raslimali; na tatu, andaa mpango utakaohitaji raslimali nyingi ili kuutekeleza. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia lazima ulete mabadiliko ya wazi katika jamii! Kwa hiyo, washiriki wanahimizwa kuandaa mpango kazi utakaowatoa katika Mtaala wa Biblia na kuwaweka katika nyanja za kanisa na jamii nzima.

**Maelezo kwa mtumiaji wa muongozo huu kuhusu kuandaa mpango kazi**

Mtaala wa Biblia wa Mazingira peke yake haukamilishi hatua ya kutoka kwenye Mtaala wa Biblia hadi hatua ya kutenda. Kwa hiyo, ni wazo zuri kuwawezesha washiriki kupata raslimali za ziada kutoka mashirika binafsi, serikali, na asasi za kijamii ili kuwezesha utekelezaji wa mpango kazi kusonga mbele.

**Ufupisho kuhusu mbinu**

Njia moja ya kufupisha maelezo kuhusu 'mbinu za mtaala' wa Biblia ni kuziweka katika miduara mitatu ukianzia na duara la kwanza ambalo ni kubwa la nje, kisha ndani yake kuna duara la kati, na hatimaye duara dogo katika duara la kati. Duara la kwanza, lile kubwa la nje, ndiyo mbinu ya Tazama-Amua-Tenda. Duara hili ndilo linalozunguka yote tunayotenda, kwa kuunganisha Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia na hatua endelevu ya 'kutafakari-na-kutenda' na kutafakari tena. Duara la pili, lile la kati lililo ndani ya duara kubwa, ndiyo mbinu ya kuanza na kujitambua kwa jamii, na kisha kuendelea na kujitambua kwa dhati kifikra, na kisha tena kurudi katika kujitambua kwa jamii. Duara la tatu, lile dogo ndani ya duara la kati, ndiyo mbinu ya kutafakari kifungu cha Biblia, kuanzia na mazingira ya 'mbele ya kifungu', kisha 'juu ya kifungu', kisha tena 'nyuma ya kifungu', na hatimaye tena 'mbele ya kifungu'.

## Sura ya 4

## Wajibu wa Muwezeshaji

Wajibu wa muwezeshaji ni jambo la msingi katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mchakato wa ushirikiano unaohitaji aina fulani ya uongozi unaowezesha. Sote tunatambua kuwa kuna mifumo ya uongozi ya ukandamizaji. Aina hizo za uongozi hazifai katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Hapa kiongozi lazima awe muwezeshaji.

Uwezeshaji ni zaidi ya ufundi; ni sanaa na ni aina ya ujuzi wa kiroho!

Wajibu wa muwezeshaji ni kusaidia lengo kuu la Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, ambalo ni ushirikiano wa kikundi. Kwa hiyo, muwezeshaji anahitaji kuwa ambaye anawezesha kikundi kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano, kwa kushirikishana raslimali zao na kusonga mbele katika kutenda jambo moja kwa pamoja.

Ili kuwa muwezeshaji wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, huhitaji sifa za kitaaluma; Uwezeshaji ni kitu ambacho Mkristo yeyote wa kawaida anaweza kufanya. Mtu yeyote anakaribishwa kuandaa na kuwezesha mtaala wowote katika kitabu hiki cha muongozo. Mitaala katika kitabu hiki cha muongozo ni myepesi kuelewa na kufuatisha, na imeandaliwa katika namna ambayo inakusaidia kuongoza kikundi katika mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

### Mchakato wa Uwezeshaji wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Vifuatavyo ni ‘vidokezo’ muhimu vya uwezeshaji, lakini kumbuka kuwa kwa kadri unavyojizoesha uwezeshaji katika mazingira ya ‘maisha halisia’, ndivyo utakavyofanya vizuri zaidi. Uwezeshaji ni ujuzi, na pia ni mazoezi ya kiroho ambayo unawezea kujifunza kwa kutenda!

1. Jambo la msingi katika uwezeshaji ni kutambua kuwa siyo suala la kiufundi tu; uwezeshaji ni ufahamu wa kiroho unaotambua mfano na sauti ya Mungu ndani ya kila mmoja.

2. Ni muhimu kukifahamu kikundi kinachoshiriki Mtaala wa Biblia. Muwezeshaji lazima afahamu mazingira ya kijamii ya kila mshiriki wa kikundi: mambo ya umri, kabila, madhehebu, lugha, jinsia [pia jinsi], mila, desturi, tofauti zao na mambo wanayofanana, ukubwa wa kikundi, nk.

   Yafaa muwezeshaji atoke katika kikundi husika; lasivyo, muwezeshaji lazima afahamu mambo halisi ya kijamii ya kikundi husika, na lazima afanye uchambuzi yakinifu wa jamii kwa kushirikiana na wanakikundi ili kwamba muwezeshaji mwenyewe aelewe matatizo halisi ya kikundi husika na jamii yake.

3. Mitaala ya Bibia ya namna hii huendeshwa kwa mtindo wa ushirikishwaji na majadiliano. Hii ina maana kwamba mitaala imekusanywa kwa kuzingatia kuwa kila mshiriki ana busara yake – mtu mmoja peke yake hawezi kuwa na ‘majibu’. Hakika, washiriki wana wajibu wa msingi na wana mchango mkubwa (pia tazama Sura ya 5). Hivyo, mtaala unapofanyika

usiwe kama darasa shuleni (muwezeshaji kama ‘mwalimu’), bali uwe kama meza ya majadiliano miongoni mwa watu waliosawa.

4. Sauti ya muwezeshaji iwe ni moja kati ya sauti nyingine ndani ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, ili kila mshiriki aweze kupaza sauti yake, hata kama mawazo yake yanatofautiana na muwezeshaji. Hii haina maana kuwa muwezeshaji hawezi kutoa mawazo yake, bali ina maana kwamba mawazo ya muwezeshaji yasionekane kuwa ndiyo yenye umuhimu zaidi kuliko wengine. Lengo kuu ni kuwezesha ushirikiano wa kikundi ili kuwa na nia moja na kufanya utekelezaji wa pamoja.

5. Kwa wanakikundi kushirikishwa katika utekelezaji wa mambo ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni muhimu sana ili kufanikisha mchakato mzima wa mtaala husika. Maelezo ya kitabu cha muongozo yanatupa kazi na wajibu unaoweza kufanywa na wanakikundi – badala ya muwezeshaji – ili kuongeza hali ya ushirikishwaji katika mtaala wa Biblia. Muwezeshaji ni lazima afahamu kazi na wajibu wanakikundi wanaweza kushiriki. Mifano ya kazi na wajibu ni kama ifuatavyo: kusoma vifungu vya Biblia; mtu wa kuandika ufupisho wa majadiliano ya mtaala kwenye karatasi za kubandika ukutani; mtu wa kuandika taarifa za vikundi vidogo; mtu wa kutoa taarifa baada ya majadiliano ya vikundi vidogo; mtu wa kufungua kipindi kwa sala; na mtu wa kufunga kipindi kwa sala.

6. Muwezeshaji anatakiwa kuwezesha ‘mchakato wa kikundi’ ufanyike. Kwa maneno mengine, inapaswa kuongoza mchakato wa kikundi, kuhakikisha shughuli zinafanywa kwa zamu, muda unazingatiwa, taarifa ya kikundi inaandaliwa tena kwa utaratibu mzuri, na kutafuta kwa namna ya ubunifu na inayojenga njia za kuwawezesha washiriki kutoa taarifa za vikundi vidogo, na kuwezesha mtaala kusonga mbele kutoka katika hatua ya kutafakari na kuingia katika hatua ya kutenda.

7. Ni muhimu kusuluhisha migogoro mara inapojitokeza miongoni mwa wanakikundi. Migogoro inaweza kuwa na faida, hivyo siyo wakati wote migogoro ni mibaya. Hata hivyo, kwa kawaida inahitaji kusuluhishwa. Mara nyingi wanakikundi wenyewe wanaweza kuimaliza migogoro, lakini wakati mwingine muwezeshaji anapaswa kuingilia kati.

8. Kwa kuwa Mtaala wa Biblia huongozwa kwa maswali, muwezeshaji anahitaji kuwawezesha washiriki kukabili maswali (na kwa njia hiyo kuweza kukabiliana wao kwa wao na pia kukikabili kifungu cha maandiko).

9. Muwezeshaji anapaswa kutoa maelezo pale tu anapoombwa kufanya hivyo, lakini katika namna ambayo inathamini mawazo ya kikundi. Kama muwezeshaji hafahamu jambo husika, au hana jibu la swali, lazima awe mkweli na aseme hajui! Ni bora kwenda kutafuta majibu kuliko mtu ajifanye anajua.

10. Ni muhimu kuhamasisha kutumia mawazo ya kawaida ya wasomaji wa Biblia wa jamii husika. Muwezeshaji lazima siku zote awe macho kutazama njia za usomaji wa Biblia ambazo kwa kawaida jamii husika inazitumia. Kutumia mawazo ya kawaida ya usomaji wa Biblia inaweza kuwa njia nzuri ya kuhamasisha wanakikundi kusoma Biblia kwa kina.

11. Muwezeshaji lazima awe macho kutambua kuwa wakati mwingine siyo wanakikundi wote wanajua kusoma. Ni wajibu wa muwezeshaji kuhakikisha kuna majadiliano na maelezo ya kutosha, hata taarifa zilizoandikwa lazima zisomwe kwa sauti, ili wale 'wanaosoma' kwa njia ya kusikiliza wanashiriki kakamilifu katika mtaala na hawaachwi nyuma.

12. Muwezeshaji anatakiwa kuhakikisha kuna muda wa kutosha kwa ajili ya majadiliano ya vikundi vidogo na utoaji wa taarifa za vikundi. Kama muda hautoshi, muwezeshaji awe mbunifu kuhakikisha kuwa kuna muda wa utoaji taarifa za vikundi vidogo. Kwa mfano, siyo lazima kila kikundi kutoa taarifa nzima kwa kila swali; badala yake, kikundi kimoja kinaweza kuanza kutoa taarifa ya majadiliano wa maswali, halafu makundi mengine yanayofuata hayana haja ya kurudi majibu yaliyokwishatolewa, isipokuwa maelezo yale tu ambayo hayajatolewa.

13. Muwezeshaji lazima auwezeshe Mtaala wa Biblia kusonga mbele hadi kufikia mwisho. Ni muhimu kukadiria muda kiasi gani utatumika kukamilisha mchakato mzima wa mtaala; kuna haja ya kutathmini makadirio ya muda kadri Mtaala wa Biblia unavyoendelea.

14. Mazoezi ya 'kuchemsha mwili' kabla ya kuanza Mtaala wa Biblia ni njia nzuri ya kuwasaidia kufahamiana. Mifano ya mazoezi ya namna hii imewekwa mwishoni mwa sura hii.

15. Kuwagawa washiriki katika vikundi vidogo ni mchakato wenye ubunifu ambao unaweza kufanywa kwa njia mbalimbali, kutegemeana na aina ya maswali ya Mtaala wa Biblia. Kwa mfano, katika Mtaala wa Biblia unaogusa masuala nyeti ya jinsia kama unyanyasaji wa kijinsia, inafaa kwa kawaida kuwagawa watu katika makundi ya akinamama peke yao, na akinababa peke yao, pia wasichana nao peke yao na wavulana peke yao. Katika mitaala mingine ambapo yafaa kuwachanganya washiriki wote pamoja, basi unaweza kutumia mazoezi ya mwili ya hapa na pale ya kuwagawa washiriki kwa muda mfupi tu, na mifano ya mazoezi husika imewekwa mwisho wa sura hii.

16. Kushiriki katika mitaala hii kunaweza amsha hisia za washiriki kwa kiasi kikubwa. Kwa sababu maada zinazojadiliwa zinaweza kuwa na maumivu au ngumu kwa watu wengi. Yafaa muwezeshaji awe tayari, na ajali mahitaji ya washiriki. Mapumziko ya chai au chakula yanaweza kutumia kwa ajili ya kupata 'mrejesho' kutoka kwa washiriki wa mtaala. Katika baadhi ya mitaala ya Biblia ni muhimu kuwa na washauri nasaha. Muwezeshaji lazima 'asikilize' siyo tu maneno yao bali pia yale wayasemayo kwa ishara ya miili yao – macho, nyuso, vidole na viashiria vingine vya miili yao.

17. Ni vizuri kufanya maandalizi kabla ya kuanza mtaala. Utahitaji yafuatayo:
    - Kusoma mtaala wote
    - Kusoma kifungu chote cha Biblia
    - Kusoma maswali yote ndani ya mtaala husika
    - Andika maelezo kwa ajili yako mwenyewe kwa kujiandaa
    - Amua jinsi utakavyowasilisha maswali ya mtaala wa Biblia: ubaoni, kwenye flipchati, na pawapointi kwa kutumia kompyuta.
    - Kusanya vitu vyote utakavyohitaji kwa ajili ya mtaala (tazama orodha ya hapo chini)

Kuna mambo kadhaa ya kiutendaji kwa ajili ya kuwezesha Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unahitaji maandalizi makini:

1. Maandalizi ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huanza na kutambua kuwa mtaala wa Biblia ni sehemu tu ya mchakato mzima mkubwa zaidi wa 'kiliturgia'/'kiroho'; Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unahusisha kuabudu, kuimba, kuomba, nk. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya maandalizi ili mambo haya yawemo katika mtaala, na kuhakikisha kuwa jamii ya mahali husika 'inaongoza' vipengere hivi vya mtaala. Katika mchakato wa Mtaala wa Biblia baadhi ya 'mazoezi haya ya kiroho' yanaweza kubeba sura mpya ya mabadiliko. Hakika, ni kusudi la Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kuleta mabadiliko katika maisha halisia ya watu, kijamii na kiroho.

2. Hakikisha una vifaa vyote vya muhimu mkononi mwako, na yakwamba vinatosha, na vinafanya kazi sawasawa. Kuna vitu ambavyo utahitaji kuvikusanya: kalamu za wino, karatasi, Biblia, karatasi kubwa (au ubao na chaki), kalamu kubwa za rangi, ubao wa kuning'iniza karatasi kubwa, gundi na pini za kushikiza karatasi. Kama utatumia pawapointi basi unahitaji laptopu, projekta, na ubao wa projecta, na nyaya za umeme za kuunganishia vifaa hiyvo. Baadhi ya mitaala ya Biblia katika kitabu hiki cha muongozo inahitaji utoe nakala ya picha kadhaa ambazo utazigawa kwa washiriki wa mtaala. Zaidi ya hayo, unaweza kutakiwa kutafuta zana nyingine kutoka katika jamii husika (licha ya muongozo huu), zana ambazo zinaweza kuwafaa washiriki kwa kuzingatia mazingira yao.

3. Hakikisha kuwa majibu yote ya washiriki na taarifa za vikundi vyao zimeandikwa kwenye karatasi ya ukutani ili wote waone. Muwezeshaji hahitaji kufanya haya yote yeye mwenyewe, yafaa aombe mtu mwingine kufanya kazi hii. Pia ni jambo zuri kuandika maswali ya mtaala kwenye karatasi ya ukutani mapema kabla ya mtaala kuanza, ili washiriki waone mara wanapofikia hatua ya kujadili maswali wakati wa mtaala. Wakati wa kuandika kwenye karatasi ya ukutani au ubaoni, yafuatayo ni muhimu yazingatiwe:
   - hakikisha mwandiko unasomeka kwa urahisi, na ni mkubwa kiasi kwamba hata mtu aliyekaa nyuma kabisa anaweza kuona – haipendezi kuona washiriki wakihangaika kusoma mwandiko.
   - Hakikisha maandishi yanasomeka na yako wazi – mara zote kuandika siyo kitu rahisi!

4. Fikiri kuhusu mahali mtakapofanyia Mtaala wa Biblia: pana ukubwa gani, kuna umeme, kuna viti, viti vinaweza kuhamishika kwa ajili ya vikundi vidogo, kuna vifaa gani humo, ukumbi una gharama sana (ikiwa utalipia), na je utakuwa ukumbi mzuri kwa ujumla kwa ajili ya Mtaala wa Biblia? Pangilia vizuri kwa ajili ya mahali pakufanyia mtaala; ni muhimu kutembelea mahali hapo na kukagua kabla ya kufanya mtaala wa Biblia.

5. Unapowezesha mtaala wa Biblia ni muhimu kuhakikisha kuwa hakuna kipingamizi chochote kati yako na washiriki. Tafadhali 'usijifiche' nyuma ya mimbari, au meza. Weka meza na mimbari pembezoni mwa ukumbi mahali vifaa viliko.

6. Yafaa kupanga ukumbi katika namna ambayo washiriki watakaa mtindo wa nusu duara na kutazamana, badala ya kutumia mtindo wa 'darasa', ambamo kila mmoja hutazama 'mbele'; siyo vizuri watu wakae nyuma ya meza. Kumbuka kuwa wajibu wa muwezeshaji ni

kuwasaidia washiriki kujihusisha kikamilifu katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, na kwa hiyo mtindo wa ukaaji ni muhimu ili kuwezesha ushiriki wao katika mtaala. Hakikisha ukumbi umeandaliwa kabla ya kuanza mtaala, ili washiriki wanapofika mtaala uanze mara moja.

Mawazo Mahususi kwa Wawezeshaji

Mazoezi ya 'Kuchemsha Mwili'

'Daladala': kwa mfano, wanaweza kuombwa 'kupanda daladala', kwa kuelekezwa idadi ya abiria wanaoweza kupanda daladala hiyo. Hivyo, kwa mfano, muwezeshaji atasema, "Panda daladala ya watu watatu watatu!" Hapa washiriki watapata muda wa kupigana vikumbo na kusukumana ili kuunda makundi ya watu watatu-watatu. Kila zoezi hili linapofanyika, washiriki katika 'daladala' hiyo wataombwa kutambulishana.

Kufahamiana: waombe washiriki kusimama wawili-wawili. Kila mmoja mtu amwambie mwenziye kitu fulani kidogo tu na kisicho cha muhimu kinachomuhusu na ambacho hakuna mwingine ajuaye. Jambo hili linaweza kuwa na maana tofauti kwa watu mbalimbali (kwa mfano 'kitu fulani kidogo tu' kinaweza kuwa mahali mama yake alipozaliwa AU rangi aipendayo). Yule mwingine asikilize kwa makini sana na kisha asema na yeye kitu fulani kidogo kinacho muhusu. Kisha kila mtu atoe taarifa kwenye kundi zima kuhusu alichoambiwa, km.: "Rehema ameniambia kuwa chakula akipendacho zaidi ni ndizi za kupika". Lengo ni kuwawezesha washiriki kujieleza kwa uhuru katika vikundi vidogo na kundi kubwa pasipo hofu.

Simu mbovu: muombe kila mtu akae kimya. Mnong'oneze mtu mmoja ujumbe mfupi. Mnong'onezee mara moja tu. Naye afanye hivyo kwa mwingie, na mwingine afanye vivyo hivyo. Kila mmoja anong'oneze ujumbe kimya kimya taratibu. Hakuna anayeruhusiwa kurudia ujumbe wake. Ujumbe uzunguke chumba chote, na mtu wa mwisho auseme ule ujumbe kwa sauti, ujumbe uliyopitia kwenye simu mbovu!

Kuwagawa Washiriki katika Vikundi Vidogo

Kuhesabu: Anza na mshiriki wa kwanza, huyu ahesabiwe kama namba 1. Mtu wa pili awe namba 2, na wa tatu 3. Kisha mtu anayefuata awe namba 1, na wa pili 2, nakuendelea. Jambo la msingi ni kumpa kila mtu namba: 1,2,2 …1,2,2 nk. Kisha wote wa namba 1 wawe kundi moja, na wa namba 2 wawe kundi jingine, nakuendelea. Hii ni njia bora kabisa ya kuwagawa washiriki katika vikundi vidogo ili kuwagawa wale waliokaa pamoja.

Kwaya ndogo: waombe washiriki waunde vikundi vidogo vya kwaya. Kila kwaya lazima iwe na sauti ya nne, tatu, pili na ya kwanza. (Njia hii ni nzuri kwa kuwagawa washiriki katika vikundi kwa kuzingatia mchanganyiko wa jinsia na umri). Baadhi ya vikundi vinaweza kuhitaji kuwa na sauti ya kwaya zaidi ya moja. Pia njia hii ni nzuri ili kuonyesha kuwa kila mtu ana sauti yake ya pekee katika ushiriki wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, na ya kwamba sote tunahitaji kusikilizana. Ingawa hii ni njia ya kugawa vikundi, usishangae kuona wengine wanaamua kuimba kiukweli!

Sura ya 5

Wajibu wa Washiriki

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia siku zote huanza na mambo ya maisha halisia ya jamii husika. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa kawaida huongozwa na mada na masuala ambayo yanagusa jamii husika. Kwa sababau hiyo, katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia wajibu wa washiriki una umuhimu sawasawa na ule wa muwezeshaji. Mtaala wa Biblia ni Mtaala wao washiriki!

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia hutumia zana za kitaaluma za kibiblia ambazo zinaweza kutoa mwanga kwa kanisa na jamii. Wasomaji wa kawaida wa Biblia ambao ndiyo walio wengi miongoni mwa washiriki wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, pia nao wana maarifa muhimu ambayo yanaweza kutoa mwanga kwa kanisa na jamii. Muongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya watu ambao wangependa kutumia utaalamu wao wa maandiko kwa ajili ya kulitumikia kanisa na jamii, lakini watu ambao wapo tayari kujifunza kutoka katika ufahamu na zana za wasomaji wa kawaida wa Biblia. Muongozo huu unahimizi usomaji wa Biblia wenye lengo la ushirikiano!

Tunaposoma Biblia huwa tunakuja na taswira ya mazingira yetu, na Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unatambua kwamba kila ufahamu wa mtu wa msingi umeumbwa na mazingira yake, na pia kwamba mazingira yetu nayo yanategemea usomaji wetu wa Biblia. Kutambua nafasi ya mazingira yetu katika usomaji wa Biblia ni jambo muhimu kwa sababu tungependa kusoma Biblia kwa wazi kabisa kwa kuzingatia na kwa ajili ya mazingira yetu. Biblia yenyewe inatuambia kuwa Mungu hunena na watu maalumu katika mazingira yao mahususi.

Lakini tunajua kuwa mazingira mbalimbali ya maisha. Kituo cha Ujamaa huzingatia zaidi mazingira ya maisha ya walio maskini, tabaka la wafanyakazi, na waliosahaulika katika jamii. Uamuzi huu unatokana na imani yetu kwamba Mungu huwajali walio masikini na wanaoonewa kwa namna ya pekee – watu ambao wamesahaulika na kunyanyaswa kijamii, kisiasa, kiuchumi au kiutamaduni. Sehemu mbalimbali katika Biblia tunasoma kwamba Mungu husikia kilio cha wajane, yatima, wanawake, wageni, wakimbizi, walemavu, maskini, na walioonewa. Yesu mwenyewe alizaliwa katikati ya maskini na akaamua kuishi na kufanya kazi na maskini; pia alikufa kama mtu aliyeonewa na kuangikwa msalabani. Kwa hiyo kuna umuhimu wa kusikiliza sauti za maskini na walioonewa katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

Watu ambao wamepata mafunzo ya Biblia na theoogia wana raslimali muhimu za kulishirikisha kanisa na jamii, lakini raslimali hizo unaweza kuona zinatumika kuwatawala na kuwanyanyasa wengine. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unautambua uzoefu wa maisha, matatizo, na raslimali za watu wa kawaida, na Mtaala wa Biblia umeundwa katika namna ambayo inawezesha uzoefu wa maisha, matatizo na raslimali za watu wa kawaida zinaweza kushirikishwa (tazama Sura ya 4). Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni mahali paushirikishaji raslimali za utaalamu wa Biblia unaojihusisha maisha ya jamii, na pia raslimali za wasomaji wa kawaida wa Biblia walio maskini, tabaka la wafanya kazi, na jamii zilizotengwa. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia una kusudi maalumu la kusoma Biblia kwa ushirikiano. Ni mchakato wa ushirikiano unaoheshimu mchango wa ‘wasomaji wa kawadia’ wa Biblia.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unaweza kufanywa hata miongoni mwa watu wenye nafasi bora katika maisha ya kiuchumi; basi katika hali hii, wajibu mojawapo wa muwezeshaji ni kuwakumbusha wale waliojaliwa kiuchumi kuhusu uhalisia wa maisha ya maskini, tabaka la wafanya kazi na watu waliosahaulika katika jamii.  Jambo hili linaweza kufanywa kwa njia ya kuwashirikisha masomo ya mtaala ambayo yamejitokeza miongoni mwa jamii maskini, tabaka la wafanya kazi na watu waliosahaulika katika jamii.

## Sura ya 5 Mfano wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Baada ya kutoa maelezo kuhusu Muongozo huu, kazi ya Kituo cha Ujamaa, mchakato wa Mtaala wa Biblia, wajibu wa muwezeshaji, na umuhimu wa washiriki wa mtaala, sasa tutatoa maelezo mahususi ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

Maelezo yanayofuata ni mfano hai wa Mtaala wa Biblia ambao Kituo cha Ujamaa kimeuongoza mara kadhaa. Maelezo haya yamewekwa ili uone mfano hai wa Mtaala wa Biblia 'jinsi ulivyo'. Mfano huu unatokana na somo la tano katika Muongozo huu, ambalo ni Marko 12:41-44.

Jamii mbalimbali zimeshafanya kazi na Kituo cha Ujamaa katika kutazama kwa kiasi gani ufisadi unaingilia mifumo na miundo ya utawala. Kwa mfano, tumeshaalikwa kuendesha mitaala ya Biblia inayotazama uzoefu wa maisha ya Wakristo wa kawaida na jinsi wanavyoonewa na mifumo ya kanisa kupitia madai makubwa ya matoleo; pia tumeshawahi kualikwa kuendesha mitaala ya Biblia inayotazama jinsi mifumo ya kiuchumi ya nchi yetu 'inavyozalisha' umaskini. Mtaala huu wa Biblia unagusa mambo haya. Tena yafaa tusisitize kwamba mtaala huu siyo jibu pekee linalopaswa kufuatwa, ila ni mfano hai wa kuonyesha mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni tendo la imani. Hivyo, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa kawaida hutawaliwa na sala na nyimbo; Hakuna linaloweza kufanyika katika mkusanyiko wa Wakristo wa Afrika pasipo kusali na kuimba kwa uhuru! Kila Mtaala wa Biblia huwa na sala na nyimbo, pia kila mtu asimamapo mbele husindikizwa na wimbo. Wakristo wa kawaida wa Afrika huamini kuwa Mungu yupo pamoja nao wakati wote, na yakwamba Biblia ni hazima ambayo Mungu huitumia kusema na watu katika maisha na mazingira yao. Kwa hiyo, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huanza na hatua ya jamii, ikiwa ni katika kuimba, kusali, mazoezi ya kuchemsha mwili, au hata fursa nyingine za kujihusisha na uzoefu wa maisha ya kijamii.

Watu wanaoshiriki vikundi vya Mtaala wa Biblia hutofautiana. Kama ilivyoonyesha hapo juu, yafaa tuwe tayari kushirikiana na waumini wa aina mbalimbali, kuanzia ngazi ya viongozi wa makanisa na viongozi wa vikundi vya wanawake. Tunapendelea kufanya kazi na vikundi vya waumini katika jamii husika vyenye nia ya dhati ya kuleta mabadiliko katika mazingira yao; hata hivyo, hatukatai mialiko ya makanisa. Katika mazingira yetu ya Afrika, mialiko ya makanisa mara nyingi inatupelekea kufanya mitaala ya Biblia kwa sehemu kubwa na wanaume tu; lakini mialiko ya vikundi vya waumini mara nyingi hutuwezesha kuendesha mitaala ya Biblia na wanawake pia.

Hapa vuta hisia kana kwamba umealikwa kushiriki Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unaoendeshwa na watumishi wa Kituo cha Ujamaa. Mtaala wa Biblia unaanza na swali lifuatalo:

Swali: sikiliza Injili ya Marko 12:41-44 ikisomwa kwa sauti. Kifungu hiki kinahusu nini?

Mtaala wa Biblia huanza na washiriki wote wakiwa katika mkutano wa pamoja. Kifungu husomwa kwa sauti na mshiriki mmoja. Jambo hili ni muhimu sana, kwa kuzingatia kuwa siku zote wapo ambao hawawezi kusoma; hawa 'husoma' Biblia kwa njia ya kusikiliza. Kisha swali

la 1 huandikwa kwenye karatasi ya ukutani, halafu muwezeshaji humuomba kila mshiriki kuongea na jirani yake kile anachodhani kuhusu maana ya kifungu cha Biblia. Baada ya dakika tano hivi muwezeshaji huomba majibu ya washiriki kuhusu swali la kwanza. Kila jibu hufupishwa na mwandishi (aliyechaguliwa miongoni mwa washiriki) na kuandikwa kwenye karatasi ya ukutani, mbele ya washiriki wote. Muwezeshaji huwa hakosowi wala kutoa maoni yoyote, isipokuwa kuwatia moyo washiriki kutoa majibu zaidi na kuomba ufafanuzi wa mshiriki kama jibu haliko wazi. Kila mshiriki akishakuwa amepata fursa kuongea (na hakuna ambaye amelazimishwa kuzungumza), mchakato huendelea mbele.

Kwa njia ya kujadiliana swali la kwanza mtu na jirani yake, kila mtu anakuwa amepata nafasi ya kuchemsha ubongo wake na yuko tayari kwa mazungumzo. Washiriki huanza taratibu lakini baadaye huongeza kasi ya mazungumzo kwa kadri wanavyogundua kuwa wana 'uhuru' wa kuongea chochote.

Yafuatayo ni majibu halisi ya wakristo wa kawaida wa Afrika Kusini (pamoja na wachungaji, wahudumu, na makasisi wao) kuhusu maana ya kifungu cha maandiko tulichotaja hapo juu: kutoa kwa uaminifu, kujitoa muhanga, umuhimu wa nia ya kweli ya utoaji, jinsi maskini wanavyotoa zaidi ukilinganisha na matajiri, nk.

Mara swali linapokuwa limejibiwa kikamilifu, na majibu yake yameandikwa na kubandikwa ukutani kuwazunguka washiriki, hatua nyingine ya Mtaala wa Biblia hufuata, ni hatua ya vikundi vidogo. Washiriki 5-7 watafanya kazi pamoja katika vikundi kwa maswali mengine yote yaliyobaki. Baada ya washiriki kufahamiana katika kikundi kidogo, basi swali la 2 huandikwa katika karatasi ya ukutani.

Swali la 2: Sasa soma Injili ya Marko 12:38-40, kifungu kinachotangulia Injili ya Marko 12:41-44. Je, kuna uhusiano kati ya 12:41-44 na 12:38-40? Kama ndivyo, ni mambo gani yanafanana?

Katika vikundi hivyo vidogo, Swali la 2 linajadiliwa, lakini lazima kila kikundi kichague muwezeshaji wake na mwandishi wake wa taarifa. Kazi ya muwezeshaji katika kila kikundi kidogo ni kuwezesha majadiliano, na kazi ya mwandishi wa taarifa ni kuandika majadiliano kwa ufupi kwa kuzingatia vipengere muhimu tu. Dakika 10 – 20 zinatosha kwa swali hili. Kwa uzoefu wetu kamwe muda huwa hautoshi! Muda ukiisha, kila kikundi huombwa kutoa taarifa ya majadiliono, kwa kuongozwa na mwandishi wa taarifa wa kikundi kwa niaba ya kikundi chote (na baada ya mwandishi kuongea, muda ukiruhusu, washiriki wengine wanaweza kuongezea maelezo katika taarifa husika). Kila taarifa ya kikundi huandikwa kwa ufupi katika karatasi za kubandika ukutani.

Katika mazingira yetu ya kiafrika, washiriki huimba (na hata kucheza) wanapoenda kwenye vikundi vyao na wanaporudi. Kazi ya vikundi huwa unawatia nguvu sana washiriki, na ishara ya kwamba wametiwa moyo hujidhihirisha katika kuimba na kucheza.

Vikundi vyote ambavyo tumewahi kushirikiana katika Mtaala wa Biblia vilionyesha kuwa kuna uhusiano kati ya Marko 12:41-44 na 12:38-40. Yafuatavyo ni baadhi ya mambo ambayo washiriki walibainisha kuwa yanafanana: katika vifungu vyote Yesu anaonyesha tofauti ya wenye nguvu na wasio na nguvu; katika vifungu vyote Yesu anaonyesha kuwa kuna tofauti ya

mtazamo namna jamii inavyoyaona mambo naye (Yesu) aonavyo; katika vifungu vyote viwili kuna hukumu; katika vifungu vyote viwili Yesu anaonyesha msimamo; katika vifungu hivi kuna uhusiano kati ya waandishi "wanaokula katika nyumba za wajane" (40) na "mjane maskini" (42). Mambo haya yenye uhusiano na mengine yametolewa taarifa na kufafanuliwa na vikundi husika.

Mpaka hatua hii utagundua tayari kuna nguvu na msisimko mkubwa katika Mtaala wa Biblia! Washiriki wanaonyesha hamu kubwa ya kwenda kwenye vikundi vyao vidogo.

Swali la 3: Sasa soma Injili ya Marko 13:1-3, kifungu kinachofuata mara baada ya Injili ya Marko 12:41-44. Kuna uhusiano kati ya 13:1-3 na 12:38-44? Kama ndivyo, kuna mambo gani yanayofanana?

Baada ya taarifa kwenye kundi la pamoja, washiriki wanarudi kwenye vikundi vyao kwa ajili ya swali la 3. Mpaka sasa wameshafahamu msingi wa swali la 3 na wako tayari kwa majadiliano ya vikundi. Muwezeshaji yafaa atoe maelezo kuhusu mgawanyo wa sura, akionyesha kuwa mgawanyo wa sura haukuwa sehemu ya maandiko ya asili, lakini uliongezwa karne nyingine baadaye, ili kuwatia moyo washiriki kuamua ikiwa mgawanyo wa sura unafaa au la. Maelezo mafupi ya namna hii yanaweza kuwa msaada katika mchakato mzima wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

Baada ya muda wa kutosha, kila kikundi kinatoa taarifa (ingawa kwa mtiririko tofauti). Kama ilivyokuwa kwenye swali la kwanza, vikundi vyote ambavyo tumefanya navyo mtaala wanaona kuna uhusiano kati ya Marko 12:38-44 na 13:1-2. Wanaona kuwa Yesu hapa pia anatofautisha na kulinganisha mitazamo inayotofautiana – mambo hayako kama vile yanavyoonekana! Zaidi ya hayo, kwa mara nyingine tena Yesu anaonyesha msimamo. Na kama ilivyo katika Marko 12:38-40, 12:41-44, hapa katika Marko 13:1-3 Yesu anashughulika na mambo ya Hekalu.

Kwa mara nyingine tena, taarifa kwenye kundi la pamoja inatoa fursa kwa kila kikundi kutoa taarifa ya majadiliano yao, ambayo yatakuwa yameandikwa kwenye karatasi za kubandika ukutani.

Swali la 4: Yesu anaingia hekaluni saa 5:27 na kuondoka saa 7:2 mchana. Katika masimulizi haya akina nani ni wahusika wakuu au makundi ya wahusika wakuu, ni kitu gani tunachofahamu kuhusu wahusika hao, na kuna uhusiano gani kati yao? Chora picha inayoonyesha uhusiano kati ya wahusika wakuu katika hekalu. Picha yako inatupa taarifa gani kuhusu masimulizi hayo kwa ujumla?

Washiriki wanarudi tena kwenye vikundi vyao na kujibu swali la 4. Swali hili linahitaji uchambuzi wa kina, ingawa ni swali ambalo watalifurahia. Kwa kawaida huwa tunatoa muda wa kutosha kwa ajili ya swali hili (dakika 30-45) na kuwahimiza washiriki kuchora picha inayoendana na majadiliano yao kwenye karatasi ya kubandika ukutani. Ufuatao ni mfano wa aina ya mchoro wa kikundi kimoja: mpambano wa mpira wa miguu kati ya viongozi wa hekalu na watu wakawaida (ikiwemo mjane masikini) wakiwa na Yesu kama muamuzi wa mchezo!

Wakati wa taarifa ya kundi la pamoja, kila kikundi kibandike picha yake na kuelezea mchoro wao. Mjadala unaofuata baaada ya mchoro kubandikwa huwa na upana na hutoa ufafanuzi zaidi wa kifungu cha Biblia. Wakati mwingine washiriki wa kikundi wanaweza kuomba maelezo ya

ziada kuhusu jambo fulani katika taarifa yao. Kwa mfano, washiriki wanaweza kuuliza Maherode walikuwa akina nani, au namna mfumo wa hekalu ulivyokuwa zama za Yesu. Wakati huu, au baadaye katika Swali la 5, muwezeshaji anapaswa kuwa tayari kuwashirikisha washiriki zana na ufahamu wake wa kitaaluma kuhusu historia na maisha ya jamii ya enzi za Biblia wakati wa Agano Jipya.

Matokeo ya mijadala ya Swali la 4 katika vikundi yanaweza kufupisha kwa ifuatavyo (kwa kuzingatia kuwa vikundi vimebainisha mambo mbalimbali kuhusu kifungu cha Biblia): Wakristo wengi wanakifahamu kifungu hiki cha injili ya Marko. Tumeshasikia hotuba nyingi na kushiriki katika mitaala kuhusu kifungu hiki. Wengi wetu 'tunajua' kifungu kinahusu nini; kinahusu kuwa wakili mwema, kutoa kwa uaminifu, kujitoa mhanga, umuhimu wa nia sahihi ya utoaji, jinsi maskini wanavyotoa zaidi ukilinganisha na matajiri, nk. Pamoja na kuwa tafsiri hizi zinagusa mambo kadhaa muhimu kuhusu kifungu hiki (12:41-44), tunatambua kuwa ni lazima tuwe tayari kuzama kwa kina ili kuliwezesha Kanisa kufanya kazi yake katika nchi yetu.

Kwanza, tunagundua kuwa yafaa kuzingatia mazingira ya fasihi na lugha ya kifungu tunachosoma. Mwanzoni tunaweza tusione uhusiano mkubwa kati ya Marko 12:41-44 na vifungu vinavyotangulia na kufuata. Hata hivyo, vinaposomwa kwa uangalifu vinaonyesha kuwa kuna uhusiano kadhaa wa wazi kati ya Marko 12:35-40 na Marko 12:41-44. Katika Marko 12:35-40 Yesu anahoji dhidi ya mafundisho (mstari 35-37) na matendo (38-40) ya waandishi. Moja ya matendo ya waandishi ambayo Yesu anawaonya wanafunzi wake na makutano kujihadhari nayo ni kwamba "hula nyumba za wajane" (40; Swahili UV). Ingawa kifungu hakiweki wazi maneno hayo yana maana gani, lakini kilichowazi katika mstari unaofuata, ni kwamba Yesu anawatazama watu wanapoweka fedha zao katika sanduku la hazina, anaona miongoni mwao yupo "mjane, maskini" (42)! Msomaji makini anaweza kuona uhusiano wa maelezo: waandishi ambao hula nyumba za wajane yamkini ndiyo sababu huyu mjane ni maskini! Mjane huyu siyo tu kwamba ni mtoaji mwaminifu; bali pia ni muhanga wa matendo ya uonevu ya waandishi. Uhusiano huu wa maelezo unatuhamisha kutoka katika kumtazama mtu mmoja (yule mjane) na kuuona mfumo mzima wa uonevu/ukandamizaji (ambao ni matendo ya waandishi wanaokula nyumba za wajane). Hapana shaka, sasa kwa kuwa tunafahamu kuwa umaskini wa mjane huyo ni matokeo ya mfumo wa ukandamizaji, ni dhahiri kwamba amejitoa kwa kiasi kikubwa katika sadaka yake. Licha ya kuonyesha jinsi mjane huyu alivyojitoa mhanga, Marko anataka pia tuone uhusiano uliyopo kati ya matendo ya waandishi na umaskini wa mwanamke huyu.

Tunapotazama vifungu vinavyofuata mara baada ya kifungu tulichoanza nacho, tunagundua uhusiano. Kwa bahati mbaya kuna migawanyo ya sura hapa, lakini tunapopuuza migawanyo hiyo ya sura tunagundua kuwa mambo mengi yanahusiana pamoja. Hivyo, tunapopuuza mgawanyo wa sura na kuendelea kusoma tunaona Yesu anaondoka hekaluni katika Marko 13:1 na kisha anatamka hukumu dhidi ya hekalu 13:2. Ni wazi kwamba Yesu amekuwa hekaluni hadi katika hatua hii ya masimulizi. Uhusiano mwingine katika maelezo unajitokeza: hali akiwa hekaluni Yesu anawashutumu waandishi; hali akiwa hekaluni Yesu anamuona mhanga wa uonevu wa waandishi, mjane maskini, akiweka fedha yake katika sanduku la hazina; hatimaye Yesu anaondoka hekaluni na kutabiri maangamizi ya hekalu. Hekalu linatajwa katika vifungu

vyote: Marko 12:35-40, 12:41-44, na Marko 13:1-2. Je kuna kitu kuhusu hekalu ambacho Yesu anakipinga? Kuna uhusiano gani kati ya hekalu na waandishi? Kuna uhusiano gani kati ya hekalu, waandishi, na watu wa kawaida ambao walikuwa wakimsikiliza kwa furaha alipowakemea waandishi? Je mazingira ya fasihi na lugha katika vifungu husika yanatupa majibu kwa maswali haya?

Swali la 4 linatupa mazingira ya fasihi na lugha ili kuchungaza maswali ya hapo juu. Yesu anaondoka hekaluni katika Marko 13:2, na kisha maudhui ya habari yanatuonyesha Yesu akijadili mambo yajayo na wanafunzi wake katika Mlima wa Mizeituni (13:3). Ikiwa hekalu habari ya msingi katika vifungu tulivyosoma, na ikiwa Yesu anaondoka hekaluni katika Marko 13:2, basi tunapaswa kurudi katika Marko ili kutafuta ni wakati gani Yesu aliingia hekaluni. Yesu anaingia hekaluni kwa mara ya kwanza katika injili ya Marko 11:11, lakini hakai muda mrefu. Jambo la kushangaza, anaenda hekaluni, anatazama tu, na kisha anaondoka hekaluni na Yerusalemu pia, na kurudi Bethania. Siku inayofuata, anarudi Yerusalem na kuingia tena hekaluni (11:15). Mara hii Yesu anatenda jambo: “akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza na kununua ndani ya hekalu, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao wauzao njiwa; wala hakuacha mtu achukue chombo kati ya hakalu” (11:15-16). Baada ya kutenda, kisha Yesu anafundisha, akisema, “Je! Haikuandikwa, ‘Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote’? Bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang’anyi” (11:17). Mara baada ya hapo tunasoma kuwa “Wakuu wa makuhani na waandishi wakapata habari wakatafuta njia ya kumwangamiza; maana walimwogopa, kwa sababu mkutano wote walishangaa kwa mafundisho yake” (11:18). Tena Yesu hakai Yerusalemu, anaondoka na kurudi Bethania (11:19). Siku inayofuata Yesu anaingia Yerusalemu na hekaluni kwa mara ya tatu (11:27), na mara hii haondoki hekaluni mpaka katika mstari wa Marko 13:2! Kwa kuwa kifungu tulichoanza nacho, yaani Marko 12:41-44, ni sehemu ya masimulizi haya yote, ni muhimu tusome masimulizi yote ya Marko 11:27-13:2 kwa uangalifu, tukizingatia fasihi na muundo wa lugha yake, ili kubainisha makusudi yake makuu.

Simulizi lote linalenga hakalu la Yerusalemu; mambo yote yanatokea katika mazingira ya hekalu. Simulizi la Marko 11:27-13:2 lina vifungu vya habari ambavyo vina mambo kadhaa yanayofanana. Simulizi linaanza na Yesu anaingia hekaluni hali akikabiliwa na wakuu wa makuhani, waandishi na wazee (11:27). Sehemu ya kwanza ya simulizi (11:27-12:12) Yesu anajadiliana na viongozi wa hekalu – wakuu wa makuhani, waandishi, na wazee. Mgogoro na uongozi wa hakalu unaonekana katika kila sehemu ya simulizi, kama tutakavyoona. Zaidi ya hayo, tunaposoma simulizi zima, ni dhahiri kwamba Yesu anaungwa mkono na makutano (12:12). Hili ni jambo muhimu katika simulizi lote: kwamba makutano wako upande wa Yesu na ya kwamba Yesu yuko upande wa makutano (tazama 11:32, 12:12, 12:37). Kitendo cha Yesu kuungwa mkono na makutano ndicho kinachowazuia viongozi wa hekalu wasifanye lolote dhidi yake.

Katika sehemu ya pili ya simulizi (12:13-17), tunatambulishwa uongozi zaidi wa hekalu, yaani Mafarisayo na Maherode. Nao tena, wanajaribu kumnasa Yesu kwa maneno, lakini aliweza kukwepa mitego yao wasiweze kumnasa. Pia anakutana na viongozi wengine tena wa hekalu katika sehemu ya tatu ya simulizi hili (12:18-27) ambapo Yesu anakabiliwa na Masadukayo, na

katika sehemu ya nne (12:28-34) Yesu anajadiliana na waandishi. Yesu anamjibu barabara mmoja wa waandishi, kwa kutambua kuwa ana nia ya dhati ya kutaka kujua Yesu ni nani na anafanya nini. Hata hivyo, baada ya majadiliano haya mapana na viongozi wa hekalu, Yesu anawageukia makutano na kuwapa uchambuzi wake kuhusu hekalu na uongozi wake. Mpaka hapa tunakuwa tumesharudi kwenye vifungu tulivyoanza navyo kwenye Mtaala wa Biblia, lakini sasa tunaviangalia kwa mtazamo wa mazingira ya fasihi na lugha ya simulizi lote kwa ujumla.

Katika sehemu ya tano ya simulizi (12:35-40) Yesu anawashutumu vikali waandishi. Kama tulivyoona, anachambua mafundisho yao (12:35-37) na matendo yao (12:38-40), kiasi cha kuwafurahisha makutano waliokuwa wakimsikiliza (12:37). Simulizi linaendelea na tunamuona Yesu anaketi karibu na saduku la hazina na kuwatazama wahanga wa mafundisho na matendo ya waandishi – na mfumo wote wa hekalu – wakitoa sadaka zao. Katika sehemu hii ya masimulizi, Yesu anajaribu kuwadhihirishia wanafunzi wake jinsi mfumo wa hekalu unavyodhulumu na kuwakandamiza watu – anawaonyesha mmoja wa wahanga, mjane maskini. Lakini wanafunzi ni wazito kuelewa, kama walivyo mara nyingi katika injili ya Marko, na kwa hiyo wanapoondoka hekaluni katika maelezo ya mwisho ya simulizi (13:1-2) wanaonekana kusifu uzuri wa jengo la hekalu. Lakini Yesu haoni uzuri huo, anaonahekalu kuwa ni taasisi ya ukandamizaji inayoongozwa na viongozi wenye dhuluma. Taasisi hii, mfumo huu, Yesu anasema, "[u]tabomolewa" (13:2), pamoja na wote ambao mafundisho na matendo yao yanaunga mkono taasisi hii; Mungu hatauvumilia mfumo wa uovu kama huu.

Mpaka sasa tumeshaielewa Marko 12:41-44 kwa namna tofauti na vile tulivyoanza. Kwa kusoma vifungu hivi vya maandiko kwa kuzingatia mazingira ya fasihi na lugha yake, kumeshatusaidia kwa upana zaidi kupata tafsiri nyingine zinazohusiana na kifungu chetu.

Swali la 5: Mfumo wa hekalu ulikuwa katika karne ya kwanza huko Palestina, wakati wa Yesu?

Tunapoombwa au tunapotoa maelezo kuhusu maisha ya jamii na historia ya kifungu husika tunafungua ufahamu zaidi wa kifungu cha Biblia. Kwa mfano, maelezo kuhusu maisha na historia ya hekalu kunasaidia kutambua kuwa hekalu lilitawala maisha ya Israeli kidini, kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Kufahamu kwamba hekalu halikuwa taasisi ya kidini tu ni maelezo yanaweza kuwasaidia sana washiriki wengi wa mtaala, na hasa wanaposoma kifungu kwa 'karibu' sana na kuanza kuona kwamba kuna mambo yenye utata 'yanaendelea' ndani ya hekalu. Kwanza, heshima na nafasi ya mtu katika jamii ilitegemea nafasi yake katika hekalu. Ukuta wa nje wa hekalu uliwatenga watu watakatifu, Israeli, dhidi ya mataifa yote. Ndani ya hekalu kulikuwa na kumbi zilizotengwa kwa ajili ya wanawake, wanaume, makuhani, na kulikuwa na Patakatifu Papatakatifu, ambapo Kuhani Mkuu aliingia mara moja tu kwa mwaka. Kimsingi, wagonjwa, wenye ulemavu wa viungo, akili na ulemavu mwingine wa mwili, pamoja na wanawake 'najisi' walizuiwa kushiriki ibada ya hekaluni.

Pili, hekalu lilitawala muda na nyakati kwa kufuata maadhimisho yake ya mwaka, kwa mfano, Siku ya Utakaso, Sikukuu ya Vibanda, Pasaka, Pentekoste, na nyingine nyingi. Kama tutakavyoona, sikukuu hizi zilikuwa msingi wa shughuli za uchumi wa hekalu. Tatu, lilitawala maisha ya kisiasa ya Israeli. Licha ya muwakilishi mkuu wa serikali ya Roma, Kuhani Mkuu alikuwa mtu wa pili mwenye madaraka makubwa zaidi wa Palestina enzi za ukoloni wa

Waroma. Kuhani Mkuu halmashauri kuu ya hekalu na baraza kuu la Wayahudi lililoitwa Sanhedrin. Wajumbe 70 wa baraza la Sanhedrin (likiwa kama aina ya bunge la Wayahudi chini ya utawala wa Waroma) kwa sehemu kubwa walitokana na wakuu wa makuhani, Masadukayo, Mafarisayo, na waandishi – wote hawa walihusika na mambo ya hekalu. Pia wajumbe wa Sanhedrin walitokana na tabaka la watawala wasiowakidini – Maherode na wazee. Kwa hiyo, makundi yaliyotajwa katika injili ya Marko siyo kwamba ni viongozi wakuu wa dini tu, hakika walikuwa ni vingunge wa kisiasa pia. Zaidi ya hayo, kuna uhusiano wa kisiasa kati ya hekalu na uongozi wake pamoja na utawala wa kikoloni Kiroma. Katika mji wa Yerusalemu, wawakilishi wa utawala wa Roma, pamoja na vikosi vyao, walikaa katika ngome ya Antonia, karibu na hekalu upande wa kaskazini-magharibi; pia katika ngome ya Antonia ndiko yalikotunzwa mavazi ya ukuhani mkuu, ikiwa ni ishara ya Waroma kuwatawala na kuwatiisha Wayahudi; na ushirikiano huu wa kisiasa ulionekana dhahiri katika uteuzi wa Kuhani Mkuu.

Hatimaye, hekalu lilitawala maisha ya uchumi wa Israeli. Hakika, kundi pekee lililokuwa kinyume na hekalu, yaani Wasene na wafuasi wa Yesu, walilenga kukosoa mfumo wa uchumi wa hekalu. Wasene, kwa mfano, waliasi dhidi ya kile walichokiona kuwa ni ufisadi wa hekalu, kwa kuwa mfumo wake uliwapendelea matajiri, na wakajikusanyia fedha na utajiri kwa kuwadhulumu watu wengine (kwa mujibu wa Andiko la Dameski). Kama somo letu linavyoonyesha, matendo ya Yesu ya kiunabii yalikuwa na sababu zinazofanana na zilizotajwa punde. Katika nchi ya Yuda, hekalu lilikuwa ndiyo taasisi ya msingi ya uchumi; ilikusanya kodi toka kwa watu, zaka, matoleo na sadaka nyingine. Sikukuu za mara kwa mara ulikuwa ndiyo wakati Wayahudi watauwa walihimizwa kutembelea hekalu na kutoa matoleo. Hazina ya hekalu ilikuwa na raslimali kubwa, na baadhi yake ilitumika kuwahudumia watu wahitaji, lakini sehemu kubwa ilitumika kununua ardhi na kukodisha. Kutokana na kodi ya hekalu iliyotozwa kutoka katika ardhi, na riba ya mikopo na madeni mbalimbali, hekalu lilikusanya utajiri mkubwa. Utajiri huu ulimilikiwa na viongozi wakuu wa hekalu, ambao tunawaona katika injili ya Marko 11:27-12:37. Kadhalika, waandishi "walikula nyumba za wajane" kwa njia mbili. Waandishi walisimamia mali ya mjane kwa niaba ya mume aliyefariki, na wakajitwalia mali nyingi kwa kutoza gharama kubwa ya usimamizi wa mirathi. Pia waandishi waliwahimiza vijana watauwa kuweka wakfu mali zao zote 'kwa Mungu'; matokeo yake yalikuwa pale wazazi wao walipotaka msaada, vijana hao walidai kuwa hawawezi kuwasaidia kwa sababu mali zao wameshaziweka wakfu kwa Mungu! Kwa njia hii waandishi "walikula" raslimali ya kijana ambayo ingeweza kumsaidia mama yake aliye mjane. Yesu anashutumu tabia hii, inayojulikana kama Kobani, katika Marko 7:9-13, na yamkini anarejea jambo hili katika kifungu chetu.

Kwa kadri Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unavyosonga mbele, washiriki wanazidi kuzama katika mazingira ya fasihi, lugha, maisha ya jamii na historia ya kifungu cha Biblia; na wanastaajabu kwamba Biblia ni raslimali yenye utajiri mkubwa, na ya kwamba wamewezeshwa kufahamu andiko kwa kina wao wenyewe. Hatua inayofuata ya Mtaala wa Biblia inawawezesha kutoa mchango wao wenyewe, kwa kuwa mtaala unaanza kulenga maana ya kifungu husika katika mazingira yetu.

Swali la 6: Fupisha mambo ya msingi unavyofahamu sasa jinsi simulizi zima la Marko 11:27-13:2 linavyotupa picha ya kifungu tulichoanza nacho (Marko 12:41-44).

Swali hili linatoa fursa kwa kundi lote kutathmini walichojifunza katika kusoma tena na tena Marko 12:41-44. Kumekuwa na majadiliano ya kina na mawazo mengi yamepatikana kutoka katika kifungu na washiriki pia. Yawezekana kila kikundi kina mkazo tofauti katika kujadili kifungu cha Biblia. Kwa mfano, baadhi ya taarifa za vikundi zimesema kuwa Yesu na mjane ni kama walimu wenza! Wote kwa pamoja, kwa namna tofauti, wanafundisha kuhusu vipaumbele vya Mungu. Vikundi vingine vimekazia wajibu wa makutano, na kusema kuwa Yesu anawapa makutano kuchagua kati ya theologia ya 'zamani' na madhara yake, na kwa upande mwingine, theologia 'mpya' na tabia mpya ya wafuasi wa Yesu. Vikundi vingine vinakazia mfumo wa uchumi wa hekalu na jinsi unavyoshindwa kuwajali waliotengwa na jamii, lakini unawapa fursa viongozi kujilimbikizia mali.

Swali hili lisiwafanye wengine wakae kimya katika kundi; badala yake swali hili lisaidie kufahamu kina cha kifungu cha Biblia na maana mbalimbali tunazoweza kujifunzag zinazoweza kutufaa wa leo.

Swali la 7: Kifungu kinatueleza nini sisi waleo katika mazingira yetu mbalimbali?

Swali la 8: Ni mambo gani unaweza kutenda ikiwa ni matokeo ya Mtaala huu wa Biblia?

Maswali haya mawili ya mwisho yanaweza kujibiwa yote kwa pamoja katika vikundi. Vikundi vinahimizwa kuandika majibu yao kwa ufupi na 'mpango kazi' wao kwenye karatasi ya kubandika ukutani. Kama muda ukiruhusu, yafaa kuwe na mrejesho kwenye kundi la pamoja ili washiriki wote waweze kusikia majibu yaliyopatikana kwenye vikundi na kujifunza kutoka katika mipango kazi mbalimbali ya vikundi.

Majibu ya maswali huwa ni ya aina tofauti kwa kuwa yanatoka katika mijadala ya vikundi tofauti. Washiriki wote huwa wanapata vitu fulani vinavyofanana kwa jinsi walivyosoma maandiko yao kwa kuzingatia mazingira yao. Kuhusu Swali la 7 baadhi ya vikundi vya Afrika Kusini vimetoa hoja kwamba ndani ya miongozo hii baada ya ukombozi, serikali ya ukombozi katika sera zake kuu za kiuchumi, zenye mlengo wa ubepari mamboleo katika mfumo wa dunia wa soko huria, hakika 'inazalisha' ukosefu wa ajira, ingawa tunaambiwa unalengo la kuongeza ajira. Wengine wanahoji kwamba miundo na mifumo katika makanisa yao, pamoja na mila na desturi zao, vinanyanyasa na kukandamiza wanyonge (wanawake, na watu waishio na VVU na UKIMWI) badala ya kuwalinda na kuwasaidia.

Katika hatua ya mpango kazi, huwa na ubunifu mkubwa unaolenga mazingira yao halisia. Mahali fulani vikundi viliamua kutengeneza liturgia ambayo inaweza kutumika kwenye ibada ya kanisa lao ili kuliwezesha kanisa kuwa mahali salama kwa waathirika na wenye VVU na UKIMWI. Vikundi vingine vilipanga hatua zaidi za kisiasa, na kuanza kushawishi serikali zao kuwa na Mifuko ya Msingi ya Jamii kwa ajili ya kuwasaidia maskini na kuwalinda kiuchumi.

Mitaala yote ya Biblia huanza na kuisha (na pia hutawaliwa) na sala na nyimbo. Mtaala ambao umeshaelezwa hapa ni Mtaala wa Biblia 'halisi', siyo maelezo tu ya kitaaluma. Maelezo yote yanadhihirisha uwezo na shauku ya Wakristo wa kawaida wa Afrika katika kujifunza Maandiko kwa kina.

Baada ya 'kufanya' Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kwa pamoja, sasa tunageukia hatua ya kutafakari mchakato wa mbinu zinazotuwezesha kufanya mtaala.

Kuitafakari Mbinu ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia hufanywa katika mfumo wa mbinu inayolenga mabadiliko ya jamii iitwayo 'Tazama-Amua-Tenda'. Mbinu hii, au mchakato, au kanuni alianzishwa na Padre Joseph Cardijn mwaka 1930 huko Ubelgiji ambako alifanya kazi ya mchungaji mlezi wa wafanyakazi wa kiwanda. Mbinu ya Tazama-Amua-Tenda imekuwa moja ya aina ya theologia ya mazingira halisia ya maisha inayoungwa mkono na wengi nchini Afrika Kusini. Mbinu hii huanza na uchambuzi yakinifu wa maisha ya jamii husika, kisha hufuata somo la Biblia, ambalo huongoza watu katika kutenda. 'Tazama' ni hatua inayohusu uchambuzi yakinifu uliyo makini wa mazingira husika ya 'maisha halisia' ya jamii, na uchambuzi huu hufanywa na makundi ya jamii yaliyojipanga ya watu waliosahaulika. Kisha 'kusudi la Mungu' la kibiblia na mapokeo ya kitheologia hutumika 'ku-Amua' kuhusu 'maisha halisia'. 'Sura' ya kusudi la Mungu kwa watu hapa duniani, kwa mujibu wa Biblia kwa msingi wa usomaji wa Biblia wa wanyonge katika jamii, hutumika kuhoji mambo ya 'maisha halisia'. Tofauti zilizopo kati ya 'sura' ya kusudi la Mungu na muonekano wa maisha halisia ya wanyonge hutoa nguvu na mwelekeo wa 'kutenda' ambao inapaswa kufuatwa kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya maisha halisia ili yapatane na mpango na kusudi la Mungu.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia kimsingi hutokana na mchakato wa Tazama-Amua-Tenda. Hakika, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni sehemu ya mbinu ya Tazama-Amua-Tenda. Kabla ya kuendesha Mtaala wa Biblia na jamii au kikundi cha kanisa, tunahakikisha kuwa ni kikundi kilichojipanga sawa, na wanakikundi wanafahamu kwa dhahiri 'agenda' yao. Kisha warsha yote inatawaliwa na wanakikundi, na siyo Kituo cha Ujamaa. Sisi tunakuja kushirikisha hazina za ziada za kitaaluma, na kuunganisha na hazina walizonazo wanakikundi. Vikundi vya namna hii kwa kawaida vinakuwa vimeshafanya uchambuzi yakinifu, na kisha vinatualika nasi ili kutafakari pamoja nao 'uhalisia' wa maisha ya jamii yao, ikiwa maisha hayo yanahusu ukatili dhidi ya wanawake, VVU, au haki ya kiuchumi.

Hapa huwa tunaweza kuchangia mambo fulani katika uchambuzi yakinifu wa jamii uliyofanywa na kikundi, kwa kutumia zana za kiubunifu kama vile tamthilia (mchezo wa kuigiza) au vipeperushi vinavyosaidia kikundi kuwa na mwelekeo fulani mahususi katika mazingira ya jamii yao. Mchango wa namna hii unaweza kutumika kama mazoezi ya 'kuchemsha mwili', ili kuhimiza ushiriki na nia ya kujifunza, na ni njia bora zaidi ya kuanzisha Mtaala wa Biblia.

Swali la kwanza katika Mtaala wa Biblia lililofafanuliwa hapo juu linaendeleza mchakato wa 'Tazama', likiwaalika washiriki kueleza ufahamu wako kuhusu kifungu cha Biblia, na linatupa mchanganuo wa wazi jinsi kundi husika linavyo-'tazama' kitheologia: "Swali la 1: Sikiliza injili ya Marko 12:41-44 ikisomwa kwa sauti. Kifungu hiki kinahusu nini?" Kwa kawaida tunajibu swali hili la kwanza kwenye majadiliano ya kundi la pamoja, washiriki wote wakiwepo. Tunasubiri kwa hamu jibu la kwanza, tunaliandika, na kisha tunaandika kila jibu linalotolewa. Wakristo wengi wa kawaida huwa hawaamini kuwa muwezeshaji angependa kujua wanawaza nini kuhusu Biblia, na kwa hiyo huwa wanakaa kimya kwa muda wakisubiri mwenye mamlaka

miongoni mwao awaambie Biblia inasema nini! Lakini huwa tunasubiri zaidi yao, na hatimaye mmoja wao anaanza kujibu. Mara tunakubali jibu lake na kuliandika. Tunaendelea hivyo hadi kufikia mtu wa tatu au wanne utaona kundi linaanza kujenga imani kwamba Mtaala wa Biblia ni 'wao'; hapo sasa huwezi kuwazuia tena; majibu yanatiririka tu. Hali hii ndiyo tunaiita kumwagika kwa roho ya 'kujitambua kwa jamii'; katika hali hii sauti za washiriki zinasikilizwa, zinakubalika, na 'zinawekewa kumbukumbu' kwenye karatasi za kubandika ukutani.

Swali la pili na la tatu huongeza kasi ya Mtaala wa Biblia. Swali la 1 huleta majibu ya haraka, lakini hapa kasi hupungua kwa kuwa washiriki wanaingia kwenye vikundi vidogo. Kama vile mpango wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia wa Glasgow usemavyo, usomaji wa mtaala wa Biblia wa mazingira halisia unapopunguza kasi ya mchakato wa ufafanuzi, huwezesha ufafanuzi wa Biblia kuwa wa kina na washiriki wanajadiliana wao kwa wao kwa makini zaidi. Ufafanuzi mwingi wa kibiblia wa 'kawaida' huwa ni wa haraka; lakini ufafanuzi wa kibiblia katika Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huwa ni wapolepole. Hivyo muda wa kutosha huhitajika ili kuendelea na kasi ya ndogo ya mchakato wa ufafanuzi. Muda kiasi gani unatumika ni jambo la muhimu sana. Ikiwa, kama mmoja wetu alivyosema, wasomaji wa 'kawaida' katika ulimwengu wa aina mbili unakinzana – ulimwengu uliyofichika na ulimwengu wa hadhara wa jamii yote – basi Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia lazima utengeneze mazingira salama ili maskini na waliotengwa wawe huru kutoa mawazo ya ulimwengu wao uliyofichika.

Swali la 2 na 3 yanawapa washiriki hali ya 'kujitambua kwa dhati' kupitia maandiko. Maswali haya yanatoa fursa ya kuchunguza uhusiano wa ndani wa sehemu mbalimbali za kifungu cha maandiko. Kalenda za masomo kanisani zinagawanya vifungu vya Biblia, lakini Mtaala wa Biblia unatusaidia kuviunganisha! Kwa misingi hiyo, kifungu kinachofahamika sana cha Marko 12:41-44, 'kimeunganishwa' na vifungu visivyofahamika sana vinavyotangulia na vinavyofuatia. Mtaala wa Biblia haufanywi kwa niaba ya washiriki, bali washiriki wanawezeshwa kuyachambua maandiko. Wakristo wengi huona shaka kuchambua maandiko. Kila siku wanachambua magazeti, radio na televisheni, ila huwa na shaka ikiwa 'wanaruhusiwa' kuchambua maandiko. Mtaala wa Biblia unawapa ruksa kuchambua na kuhoji maandiko.

Swali la 4 linatoa nafasi zaidi ya kuchunguza mazingira ya lugha na fasihi ya zimulizi lote ambalo ndani yake kuna kifungu cha Marko 12:41-44. Marko mara nyingi hubadilisha maudhui ili kuashiria na kutofautisha simulizi moja hadi jingine; kwa hiyo kuwaonyesha washiriki kiashiria hiki cha simulizi katika Marko 11:27, Yesu anapoingia hekaluni, hadi Marko 13:2, Yesu anapotoka hekaluni, ni zana ya ufahamu ambayo wasomaji wa kawaida wa Biblia waliowengi wanaweza kuwa hawana. Pia ni zana ambayo inatusaidia kuunganisha pamoja vifungu vyenye maana moja katika injili ya Marko. Kadhalika, Swali la 4 linavunja kanuni ya utoaji taarifa ya vikundi kwa maneno; na badala yake taarifa ya vikundi vidogo inakuwa kwa njia ya mchoro. Tena vikundi vinaweza kutoa taarifa kwa njia ya mchezo wa kuigiza kama kuna muda wa kutosha kufanya hivyo.

Michoro hii inabandikwa ukutani ndani ya ukumbi wa warsha pamoja na karatasi za ukutani zenye taarifa za mkutano wa pamoja na taarifa za vikundi vidogo kwa ajili ya Swali la 3 na Swali la 4. Washiriki wanakuwa wamezungukwa na maneno yao na michoro yao!

Swali la 5 linahusiana kwa karibu na Swali la 4. Katika michoro yao, baadhi ya vikundi wataeleza ufahamu wao wa maisha ya kijamii na historia ya hekalu, au wanaweza kuuliza. Swali la 5, linatuwezesha kuchunguza mambo hayo na kushirikishana. Kwa Wakristo wengi wa kawaida 'kile kilichotokea hasa' wakati wa Yesu kina umuhimu. Wanapenda kujua ulimwengu wakati wa Yesu ulikuwaje na unafananaje na ulimwengu wetu wa leo.

Kama maelezo ya Mtaala wa Biblia yalivyo hapo juu, tunatumia mtazamo maalum wa kitaaluma wa kibiblia tunapotoa maelezo ya mazingira ya maisha ya jamii na historia ya kifungu cha maandiko kwa jamii husika tunapoongoza mtaala. Maandiko ya wanataaluma kuhusu mazingira ya maisha ya jamii na historia ya sasa na wakati wa Biblia hutufaa katika Mtaala wa Biblia. Maisha yetu ya 'ulimwengu wa tatu' yanatawaliwa na miundo ya ukandamizaji wa 'kimfumo'.

Swali la 6 ni swali la ufupisho: "Swali la 6: Fupisha mambo ya msingi unavyofahamu sasa jinsi simulizi zima la Marko 11:27-13:2 linavyotupa picha ya kifungu tulichoanza nacho (Marko 12:41-44). Swali la namna hii linawezesha kila kikundi kukusanya mawazo na majadiliano yao, na linaweza kuulizwa kwa njia mbalimbali. Sisi wakati mwingine huwa tunawauliza washiriki kama wangetakiwa kutuma ujumbe mfupi wa simu 'sms' kwa rafiki zao kuhusu Mtaala wa Biblia wangesemaje.

Swali la 7 na 8 linaelekeza Mtaala wa Biblia kutoka katika 'Kuamua' na 'kujitambua kwa njia ya kujichambua kwa dhati' kuelekea 'Kutenda' na 'jamii kujitambua'. Mtaala wa Biblia ni wa jamii husika, na kwa hiyo kipengere hiki ni nyeti, kwa kuwa washiriki hupaswa kuyaweka katika matendo yale waliyoyasoma katika maandiko. Kila kikundi hutoa taarifa ya mpango kazi ukiwa umeandikwa kwenye karatasi za kubandika ukutani kama njia rasmi ya kujituma kutenda. Mtaala huu wa Biblia ni mchakato wa ushirikiano kati ya Wakristo wa kawaida katika jamii za wanyonge na wataalamu wa Biblia. Ni mchakato unaohusu kushirikishana zana na mapambano kwa ajili ya mabadiliko ya jamii.

Katika Kituo cha Ujamaa tunasema ili kuendesha Mtaala wa Biblia unapaswa kuzaliwa upya, mara ya pili! Kwa mara ya kwanza tunazaliwa "kutoka juu" kwa mujibu wa Yohana 3:3. Mtaala wa Biblia unatulazimu wanazuoni tuzaliwe mara ya pili "kutoka chini". Harakati za kuishi kwetu, ukombozi, na maisha tele kwa wote, zinatutaka tushirikiane na harakati za jamii za wanyonge; ushirikiano wetu ndiyo unafanya tualikwe kuendesha Mtaala wa Biblia katika jamii husika. Hivi ndivyo Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ulivyoanza katika jimbo la KwaZulu-Natal, Afrika ya Kusini miaka ya 1980. Hivi ndivyo Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia unapaswa kusonga mbele katika mapambano yetu ya ulimwengu ili 'ufalme' wa Mungu uje duniani, kama ulivyo mbinguni.

Katika ukurasa ujao, wasomaji watapata maelezo kuhusu mbinu ya Mtaala wa Biblia. Mengi yamejadiliwa tayari, lakini yamewekwa tena ili kutukumbusha na kutoa ufafanuzi zaidi. (Kwa maelezo zaidi tazama makala hii: West, Gerald O. "Do Two Walk Together? Walking with the Other through Contextual Bible Study." *Anglican Theological Review* 93, no. 3 (2011): 431-49).

Mbinu ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Aina mbili za maswali hutumika katika mchakato wa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia:

- Maswali yahusuyo Mazingira Halisia na utambuzi wa jamii – huzingatia uzoefu, raslimali, na hisia za jamii, kadhalika jinsi maandiko yalivyoifikia jamii (k.m., swali la 1, 7, na 8).

- Maswali yahusuyo uchambuzi wa kujitambua kwa dhati kibinafsi na uchambuzi wa maandiko – ni maswali yanayotokana na zana za kitaalam za kibiblia zilizopangwa na kuanishwa kitaaluma (k.m., maswali ya 2-6).

Aina mbili za uchambuzi wa maandiko hutumika katika usomaji wa Biblia:

- Usomaji wa Biblia unaozingatia sarufi na fasihi ya lugha unatumika kuwezesha kusoma kifungu cha Biblia kwa uangalifu na kwa makini. Hapa tunazingatia uhusiano wa maelezo ndani ya kifungu; mwanzo na mwisho wa kifungu, wahusika, maudhui, kusudi, nafasi ya msimulizi, nk. Wasomaji wa kawaida hawasomi Biblia kwa mtindo huu, hivyo hii ni dhana ya nyongeza wanayoweza kuitumia.

- Usomaji wa Biblia unaozingatia historia na maisha ya jamii unatumika kuchunguza uhusiano uliyopo kati ya kifungu cha Biblia na mazingira ya ulimwengu ambamo kifungu kiliandikwa. Kwa hiyo tunachukunguza ulimwengu uliyo 'nyuma ya kifungu': asili ya historia yake, mwandishi, tarehe, na uchambuzi wa mazingira ya maisha yaliyosababisha kifungu kiandikwe; yaani uchambuzi wa kijamii, kimila, kiuchumi, kisiasa, na kidini.

Huwa tunaanza na usomaji wa Biblia unaozingatia sarufi na fasihi ya kifungu kwa sababu mbili:

- Kwa sababu kwa mtindo huu wote tunaweza kuyafahamu maandiko sawasawa, pasipo kutegemea wataalamu wa maandiko kwa kiasi kikubwa.

- Kwa sababu maswali yahusuyo historia na maisha ya jamii ambayo hufuata huwa ni maswali ya watu husika na siyo ya wataalamu wa maandiko.

Wajibu wa mtaalamu wa Biblia ni 'kusoma na' watu, na siyo 'kuwasomea' watu. Hivyo tunapaswa kuwezesha mchakato wa usomaji kwa kuuliza maswali zaidi kuliko kutoa majibu. Maarifa ni nguvu, na yanamilikiwa na watu. Watu wa kawaida lazima wagundue kwamba wao pia ni chanzo cha maarifa; jambo hili litawapa nguvu.

Kupokea mrejesho na kukubaliana na majibu yao ni jambo la muhimu. Watu wa kawaida ni mara chache wanapata nafasi ya kusema yaliyo myoyoni mwao. Kuyaandika majibu yao ubaoni au kwenye karatasi ukutani ni njia ya kuwatia moyo na kuwajengea uwezo.

Maelezo na kumbukumbu mijadala yafaa zitokane na mchakato wa Mtaala wa Biblia ambao ndiyo sauti ya washiriki. Maelezo na kumbukumbu hizi ni zana muhimu kwa sababu zinawakilisha maendeleo ya usomaji, ufafanuzi na theologia ya watu husika katika mazingira yao.

Mtaala wa Biblia ni mchakato wa mabadiliko ya jamii na jumuiya husika, na lazima kuwe na matokea ya namna mbalimbali ya kujipanga na kutenda.

Ufupisho wa Maswali

1. Soma Marko 12:41-44. Kifungu kinahusu nini?

2. Sasa soma Marko 12:38-40. Kuna uhusiano gani kati ya 12:41-44 na 12:38- 40?

3. Sasa soma Marko 13:1-2. Kuna uhusiano gani kati ya 12:41-44 na 13:1-2?

4. Yesu anakuja hekaluni saa 5:27 na kuondoka saa 7:2. Wahusika ni akina nani, na kuna uhusiano gani kati yao? Chora picha ya uhusiano.

5. Hekalu lilikuwa na wajibu gani katika karne ya 1 huko Palestina.

6. Fupisha kwa kutumia tungo moja kueleza Marko anasema nini katika Marko 11:27-13:2.

7. Kifungu hiki kinasema nini katika mazingira yako?

8. Ni mambo gani unaweza kupanga kuyatekeleza kutokana na Mtaala huu wa Biblia?

Muhtasari wa Mbinu ya Mtaala

- Maswali yahusuyo ufahamu wa jamii, yanayozingatia uelewa wa washiriki na zana zao za kutafsiri maandiko

- Maswali yahusuyo ufahamu yakinifu wa maandiko, yanayozingatia kusoma kifungu cha Biblia kwa uangalifu na kwa makini.

- Ufafanuzi wa dhati wa maandiko

- Mbinu hii inatumia ubunifu wa washiriki wa Mtaala

- Mbinu inatumia maswali yahusuyo historia na maisha ya jamii kwa kuzingatia mawazo ya washiriki; inatutoa katika taarifa za ‘ndani’ za kifungu na kutupeleka ‘nje’ ya kifungu

- Ufupisho unawasaidia washiriki kutambua ufahamu wao wa kifungu cha Biblia

- Mbinu hutumia maswali yahusuyo ufahamu wa jamii, yanayozingatia uelewa wa washiriki na zana zao za kutafsiri maandiko

- Mtaala wa Biblia huanza na hatimaye humaliza na ufahamu wa jamii, yaani jamii kujitambua

- Mtaala wa Biblia humilikiwa na jamii husika

Sura ya 6

Mfano wa Kuandaa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Mfano huu unatumia maisha halisia na mazingira yahusuyo VVU.

Tazama: Mchakato wa kuandaa Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia huanza na hatua ya 'Tazama'. Uchambuzi yakinifu unaweka bayana, kwa mfano, swali kuhusu 'sababu' za VVU na inatoka wapi – yaani kuhusu VVU kuwa ni 'ugonjwa wa wenye dhambi', ni 'mshahara wa dhambi' – hili ni swali la msingi.

Amua: Mara baada ya uchambuzi yakinifu wa mazingira ya VVU, Mtaala wa Biblia huchochea mjadala kati ya 'uhalisia' wa maisha na 'zana' za Biblia ili kuleta ufafanuzi wenye ukombozi. Changamoto ni kupata Mtaala utakao jibu swali kuhusu 'sababu'. Hapa tutatumia Yohana 9, tukizingatia 'muundo' wa kifungu.

Tenda: Mtaala huanza na mchakato unaoelekea kwenye utekelezaji kwa njia ya kuwa na mpango kazi, lakini utendaji halisi hufanyika katika maisha ya jamii. Kwa hiyo Mtaala kazi yake ni kuibua mpango wa utendaji unaoweza kutumika katika kanisa ili kukosoa tabia ya unyanyapaa kwa wenye VVU.

Kinachofuata katika mfano huu ni aina ya Mtaala unaoweza kutumika ili kuzungumzia VVU katika mazingira yetu. Kadri unavyoendelea na mfano huu, fikiria tena 'mfumo' wa Mtaala wa Biblia. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, kama tulivyoona, unafuata mfumo maalumu. Tumelieleza jambo hili kwa namna kadhaa. Kwa kifupi, Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia hufuata hatua nne:

1. Mtaala wa Biblia huanza na huzingatia sauti na mtazamo wa jamii, kwa kutumia maswali yenye mada za mazingira husika, kama vile "kifungu kinahusu nini?" Kama kifungu kinafahamika, basi majibu ya swali yataibua kile ambacho washiriki wanafahamu kuhusu kifungu husika, kutokana na uzoefu wao wa kusoma Biblia na misingi ya imani ya madhehebu yao. Kama kifungu hakifahamiki vizuri, basi majibu yatatokana na taswira ya washiriki mara baada ya kusoma kifungu katika Mtaala husika.

2. Hatua ya kwanza ya Mtaala ni kuainisha mada za kifungu kwa kuzingatia mazingira ya jamii husika; hatua ya pili huwa ndefu na inazingatia kwa makini sarufi na fasihi ya kifungu husika. Maswali yahusuyo kifungu huwazamisha washiriki katika ulimwengu wa Biblia na kifungu husika. Muundo wa maswali hutegemea aina ya kifungu kinachosomwa. Kama kifungu ni simulizi, basi maswali yatahusu, kwa mfano, wahusika na uhusiano wao katika simulizi. Kama kifungu ni cha ushauri, basi maswali yatahusu muundo wa shairi na dhana au taswira zinazojitokeza. Kama kifungu ni barua, basi maswali yatahusu maudhui na hoja ya barua. Kwa hiyo hatua ya pili huzingatia uchambuzi wa kifungu, kwa kuzingatia mfumo wa matumizi ya lugha katika kifungu.

3. Hatua ya tatu huwatoa washiriki katika sarufi, muundo na fasihi ya lugha na kuwaingiza katika kuchambua ulimwengu wa Biblia, historia na jamii ambayo kifungu kinazungumzia. Kila kifungu cha Biblia 'kinahusika' na ulimwengu halisi, ambamo kifungu kilitokea. Kila kifungu

cha Biblia kina mazingira ya aina tatu, kwanza, muundo wa lugha, sarufi na fasihi; pili, historia na maisha ya jamii enzi za ulimwengu wa Biblia; tatu, mazingira ya msomaji wa Biblia na jinsi anavyohusianisha kifungu cha Biblia, ulimwengu wa 'kale' na maisha ya ulimwengu wa msomaji. Maswali hutumika ili kuchunguza historia na maisha ya jamii ya ulimwengu uliyo 'nyuma' ya kifungu cha Biblia. Kwa mfano, maswali kuhusu wajibu wa hekalu la Yerusalemu wakati wa Yesu, hutupa maelezo ya kutuwezesha kuelewa maelezo ya Marko 12.

4. Hatu ya nne na ya mwisho inahusu mazingira ya washiriki. Mazingira yao sasa hupewa kipaumbele. Maswali kuhusu mada zinazogusa mazingira halisia huwatoa washiriki kutoka katika ulimwengu wa Biblia na kuwaingiza katika maisha halisia ya ulimwengu wao. Wanajikuta kifungu cha Biblia 'kinazungumza nao' katika ulimwengu wao, na kuwataka kutenda na kuleta mabadiliko ya jamii.

Kwa mfano

Uchambuzi wa maswali

1. Sikiliza Yohana 9:1-41, na mshirikishe mtu aliyekaribu nawe jinsi kifungu hiki kinavyotafsiriwa katika mazingira yako.

2. Yesu anajihusisha na mtu aliyezaliwa kipofu kwa namna kadha: Yesu alimuona (mst.1); Yesu akamgusa (mst.6); Yesu akaongea naye (mst.7); Yesu alimtafuta (mst.35); Yesu anazungumza naye na kumrudisha katika jamii (mst.35-41). Soma tena na tena mistari hii; mistari inatuambia nini kuhusu Yesu na mtazamo wake kwa mtu huyu aliyezaliwa kipofu? Chora picha inayoonyesha Yesu akikutana na mtu huyu.

3. Swali wanalouliza wanafunzi wa Yesu katika mstari wa 2 linaonyesha jinsi walivyofundishwa kuhusu dhambi na magonjwa. Ni mafundisho gani hayo? Mtazamo wao ukoje?

4. Anachosema Yesu mstari wa 3, na kile anachofanya (tazama swali la 2 hapo juu) vinatoa mafundisho mbadala. Ni mtazamo gani huu mbadala wa kitheologia?

5. Mtazamo wa kanisa lako unasemaje kuhusu wenye VVU? Unafanana na Yesu au ni kama mtazamo wa wanafunzi?

6. Katika mazingira yako utajibuje kuhusu Mtaala huu wa Biblia? Km. ni kwa namna gani unaweza kuhubiri kuhusu VVU na UKIMWI katika namna ambayo inapinga mtazamo wa kitheologia unaoaminiwa na wengi kwamba VVU ni adhabu toka kwa Mungu? Ni mambo gani yanayopaswa kubadilishwa katika kanisa unaloabudu ili wenye VVU waone wanakubalika?

Maswali ya ufahamu wa jamii. Kifungu hiki ni kirefu, kimejaa mjadala. Kukiwa na maandalizi mazuri kifungu hiki kinaweza kuwa na nguvu sana kikisomwa kwa mtindo wa kuigiza.

Maswali ya kujitathmini kupitia maandiko. Zana za kisarufi, fasihi na muundo wa lugha hutolewa kwa washiriki, kuonyesha mpangilio na mfumo wa masimulizi ya Yohana.

Unaweza kuuliza: kwa jinsi gani Yesu anajihusisha na mtu aliyezaliwa kipofu? Lakini, kwa njia ya kuwapa mpangilio wa masimulizi, unasaidia kuongeza kasi ya mchakato wa Mtaala na kuwawezesha washiriki kuchunguza kifungu kwa kina. Simulizi linaanza na Yesu 'kumuona' mtu aliyezaliwa kipofu, kwa hiyo Mtaala huanza na Yesu katika Swali la 2. Kisha tunahamisa kwa wanafunzi; swali lao ndilo swali la makanisa yetu! Ingawa mkazo bado uko kwenye simulizi, hatua hii inaweza kuwa ni fursa ya kujadili mawazo mbalimbali kuhusu magonjwa na mateso wakati wa Yesu. Swali hili ni muhimu kwa kuwa linawawezesha washiriki kutafakari msingi wa hoja ya Yohana 9. Inaonekana Yesu anaonyesha kwamba wanafunzi wanauliza swali lisilosahihi! Swali sahihi ni hili: 'Tukimuona mtu aliyezaliwa kipofu tutafanya nini?'

Hapa Mtaala unarudi tena nyuma kwenye swali la ufahamu wa jamii. Kwa kuwauliza washiriki kulinganisha mtazamo wa Yesu na ule wa wanafunzi wake, unawawezesha kuona kwamba majibu yao na majibu ya makanisa yao 'hayafanani na ya Yesu'.

Swali hili linaweza kuulizwa kwa upana zaidi: 'Sasa utafanya nini kutokana na Mtaala huu wa Biblia? Hata hivyo, maswali mahususi kama haya huwasaidia washiriki kujiandaa kwa ajili ya mabadiliko.

Yohana 9, Sehemu ya 2

Mtaala huu wa Biblia hautupatii utajiri wote wa kifungu. Kuna wahusika wengine katika simulizi na kuna mahusiano zaidi kati ya wahusika ambayo tunaweza kujifunza kwa kina na kwa uangalifu zaidi. Jambo hili linaweza kufanyika kwa ubora zaidi katika sehemu ya pili ya Mtaala wa Biblia.

Kwa njia ya kufanya Mtaala wa Biblia wa Yohana 9 kwa sehemu mbili tunaweza kuona jinsi tunavyoweza kuhusianisha mada katika Mitaala inayochukua warsha zaidi ya moja.

Ufuatao ni muhtsari wa sehemu ya pili ya Mtaala wa Biblia wa Yohana 9, kwa kufuata mbinu sawa na ile iliyotumika hapo juu.

Uchambuzi wa Maswali

1. Someni kifungu kwa pamoja tena. Kisha kwa pamoja andikeni kwa ufupi mambo mliyofanya na kuyagundua kwenye Mtaala wa kwanza.

2. Kuna makundi mengine manne ya watu waliyojihusisha na mtu aliyezaliwa kipofu: majirani zake na watu waliyomfahamu (mst.8); Mafarisayo (mst.13); wayahudi/viongozi wa Wayahudi (mst.18,24); wazazi wake (mst.20). Wanajifunza nini kuhusu makundi haya na mitazamo yao kwa mtu aliyezaliwa kipofu?

3. Ni upi mtazamo wa kitheologia wa Mafarisayo na viongozi wa Kiyahudi?

4. Ni kitu gani kinawazuia wajirani na familia wasishikamane na mtu huyu aliyezaliwa kipofu?

5. Kifungu hiki kinatufundisha nini kuhusu mazingira yetu ya VVU?

6. Tunawezaje kupinga unyanyapaa na ubaguzi katika makanisa na familia zetu?

Ni njia bora zaidi ya ‘kukumbuka’ na kushiriki kwa upya kile kilichofanyika katika Mtaala wa Biblia uliyopita. Hatua hii inasaidia washiriki kurejea mambo nyeti zaidi kutoka katika Mtaala wa Biblia.

Wahusika tuliyowaona sehemu hii ya pili hawakujadiliwa kwa kina kwenye Mtaala uliyopita. Wanatupa fursa kuona mitazamo mingine ya kitheologia; na mifano mingine ya unyanyapaa na ubaguzi.

Hali hii inatupa ‘nafasi’ ya kujadili zaidi theologia ‘zinazohusu’ VVU na UKIMWI.

Jambo hili ni muhimu sana katika jamii zetu. Linatusaidia kuchambua jinsi unyanyapaa na ubaguzi ‘unavyoathiri’ watu wote.

Maswali mawili ya mwisho yanatoa fursa zaidi kusikia changamoto ya kifungu cha Biblia na kuitikia changamoto hiyo.

Neno la mwisho kuhusu ‘muundo’

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni usomaji wa Biblia unaozingatia mazingira na maisha halisi ya watu wa kawaida, hasa maskini na waliosahaulika. Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ni usomaji wa Biblia unaozingatia dhima, lugha pamoja na historia na maisha ya jamii, na hasa kuwezesha sauti za maskini na wanaobaguliwa kusikika. Muundo huu wa Mtaala ndio unaozingatiwa katika kazi yetu na jamii.

Sura ya 8

## Kueleza, kumiliki na kurasmisha theologia ya jamii: hitimisho kuhusu faida ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

### Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo kuhusu matokeo ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia, yaani uwezo wake wa kuiwezesha jamii ya maskini na waliosahaulika kuieleza theologia yao.

Kutotambua shughuli za wanaharakani katika jamii kuwa ni sehemu ya theologia 'rasmi' ya kanisa, ni moja kati ya dalili ya udhaifu wa kanisa katika kueleza na kurasmisha theologia ya jamii inayotokana na mapambano ya ukombozi ya miongo mingi.

Kwa kuzingatia uchambuzi wa Walter Brueggeman, theologia 'rasmi' ya kanisa, huwa na mlengo wa kuhalalisha na kuimarisha mfumo wa kanisa husika. Theologia ya kanisa huwa ni harakati ya kuthibitisha mfumo ambao umejikita miongoni mwa wachache waliojiimarisha na kwa usalama wao, pia ni theologia ambayo inamueleza Mungu katika namna ya kutetea utarabibu uliwekwa (Brueggemann 1993:202). Katika Waraka wa *Kairos*, hii ni "Theologia ya Kanisa" ambayo haijali maswala ya siasa na jamii (theologians 1986). Kwa mujibu wa Charles Villa-Vicencio, ubaya wa theologia hii huzalisha imani ya kidini yenye msimamo mkali (Villa-Vicencio 1989:16).

Ipo theologia nyingine inayohoji theologia ya kimapokeo, theologia hii huwa ni harakati ambayo imejikita miongini mwa wacheche wenye mlengo wa mabadiliko, na ambao wanamwelezea Mungu kuwa mwenye kuingilia kati hata katika taasisi, mifumo na utaratibu usioingilika (Brueggemann 1993:202). Kwa kutumia maneno ya Waraka wa *Kairos*, hii ni "Theologia ya Unabii", ingawa ipo katika kanisa, bado haihesabiwi, na yamkini yaitahesabiwa kamwe, kuwa ni sehemu ya theologia rasmi ya kanisa. Hata hivyo, changamoto iliyobaki ni kutafuta njia ya kuziwezesha theologia za unabii zinazotokana na harakati za mapambano ya ukombozi ili zipenye na kubadili mfumo wa theologia kandamizi.

### Nadharia na Vitendo – kutenda na kutafakari

Ingawa kanisa linapaswa kulaumiwa kwa kutowawezesha wanaharakati wa kikristo kuwa na theologia ipasayo kwa kazi yao, wanaharakati na taasisi zao wanaweza laumiwa pia. Sisi tunaojihusisha na harakati za mabadiliko tumekuwa mafundi sana wa kutenda, lakini tumepuuza umuhimu wa kuwa na wakati wa kutafakari kitheologia yale tuyafanyayo. Kwa maneno mengine, kazi yetu inategemea uchambuzi yakinifu wa jamii, lakini siyo uchambuzi yakinifu wa jamii pamoja na injili!

Nadharia tendwa ina hatua mbili: hatua ya kutenda na hatua ya kutafakari, ni hatua zinazofuatana moja baada ya nyingine katika namna ya mzunguko kwenye duara. Wanaharakati wameshindwa kuwa na muda wa kutosha, nafasi na zana ili kuwawezesha kutafakari. Matokeo yake ni wanaharakati 'kuchoka' na kufilisika kitheologia, na kisha kubaki katika theologia iliyozoeleka, ambayo kwa kawaida huwa ni ile ifananayo na theologia ya kiinjili inayohalalisha mfumo fulani.

“Theologia ya Kanisa” ndiyo tunayoipata hata kwa wanaharakati katika sekta za serikali. Mmoja wa wanatheologia wa Afrika Kusini aliposoma andiko hili alisema watu wengi wa Afrika Kusini wenye kipato wanaipenda “Theologia ya Kanisa” kwa sababu inawasahaulisha harakati zao za ukombozi na kuhalalisha mfumo legevu wa kiutawala uliyopo.

Katika lawama hizi, hatupaswi kuwaacha watheologia na wataalamu wa Biblia. Kama asemavyo Albert Nolan (Nolan 1996) kwamba wafanyakazi wa kawaida (pamoja na wasio na ajira na wanawake vijijini) hawana muda, nafasi na zana za kuitendea kazi theologia katika nyanja za maisha yao. Wanawahitaji watheologia na wataalamu wa Biblia wanaojihusisha na mabadiliko ya jamii ili waungane nao na kuitendea kazi theologia, kwa kuwashirikisha muda na zana zao. Kwa hiyo wataalamu wa Biblia na watheologia ambao hawawezi kujitoa namna hii basi lazima walaumiwe kwa kusababisha mazingira ya kitheologia yaliyofilisiki.

Theologia ya maisha ya jamii

Baada ya kusema hayo, singependa ieleweke kwamba wakristo wa kawaida na wanaharakati hawana theologia wanayoifanyia kazi. Wanayo theologia! Hata hivyo, wanaifanyia kazi theologia kwa njia ya maisha yao, na mara nyingi siyo kwa maelezo ya ufafanuzi wa theologia (Cochrane 1999). Wanayo ‘theologia itendayo kazi’ kwa njia ya maisha yao. Tatibo ni kwamba ‘theologia ya maisha ya jamii’ mara nyingi haihusishwi na theologia ya kanisa. Kwa hiyo tatizo siyo kutokuwepo kwa theologia ifaayo ya jamii, bali ni kupuuzwa na kuitenganisha theologia ya unabii, yaani theologia inayokubali maumivu (kwa kutumia usemi wa Brueggemann’s), na ile theologia kandamizi za kanisa.

Swali lililobaki ni hili, kwanza, kwa jinsi gani tunawezesha kuieleza na kuimilikisha theologia ya maisha ya jamii, na pili, kwa jinsi gani tunafanya theologia za jamii zikubalike kwa umma kama theologia rasmi – hatua hii ndiyo inaitwa kurasimisha, dhana hii inatoka kwenye taaluma ya elimu, yaani kubainisha mambo muhimu yasiyofundishwa na kuyafanya kuwa sehemu ya mtaala wa elimu.

Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia

Namna ya kufanya Mtaala katika mazingira mbalimbali ya ulimwengu, na kwa njia mbalimbali, ni kwa njia ya Mtaala wa Biblia unaozingatia jamii. Hapa hatukusudii kueleza historia na makundi ya mitaala. Mifano ifuatayo inatosha kuueleza mbinu za Mtaala wa Biblia inayozingatia jamii: *Centro de Estudos Biblicos* (CEBI) ni mtaala wa Biblia wa Brazili ambapo wataaluma watakao mabadiliko kama vile Carlos Mesters (Mesters 1984; 1989) walifanya kazi ya mtaala unaotumia mbinu ya “Pande Nne” iliyobuniwa na Gilberto Gorgulho; mbinu ya Tazama-Amua-Tenda ya Wafanyakazi Vijana wa Kikristo (YCW) na Taasisi ya Theologia ya Mazingira ya Maisha Halisia (ICT) (Stevens 1985; Dumortier 1983; Speckman and Kaufmann 2001:4; Cochrane 2001:77); Mtaala wa Biblia wa Jamii ya Ilimo (Philipott 1993); na mbinu ya Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia ya Taasisi ya Mtaala wa Biblia na Huduma kwa Wafanyakazi (ambayo kwa sasa inaitwa Kituo cha Ujamaa) (West 1995, 2003).

Jambo linalojitokeza katika mbinu hizi zote ni kwamba zinawapa watu nafasi salama ambamo maswala yaliyofichika au kufichwa (Scott 1990) yanaweza kuelezwa na kumilikiwa; zinatoa

nafasi salama ya kushirikishana zana za jamii na za kitaaluma kwa ajili ya kuisikia na kuieleza theologia ya maisha ya jamii, na kuwezesha mchakato unaowezesha washiriki kuchambua na kujimilikisha theologia zao za maisha ya jamii (kwa maelezo zaidi tazama West 2003). Sehemu ya 2 ya Mtaala ndiyo huwezesha uchambuzi, umiliki na uelewa kwa lengo la kurasimisha theologia (West 2003; Haddad 2000; Nadar 2003).

Mada ya maisha halisia

Mada zifuatazo za maisha halisia zitatupa taswira ya mazingira halisi ya maelezo yaliyotolewa kuhusu Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia.

Mada ya 1: Ukatili dhidi ya wanawake

Kwa kuzingatia hali halisi ya ukatili dhidi ya wanawake katika mazingira yetu, tangu mwaka 1996 Kituo cha Ujamaa kinatumia katika Mtaala wa Biblia habari ya Tamari (2 Samweli 13:1-22) kama zana ya kuelezea, kumilikisha na kurasimisha theologia ya maisha ya jamii inayotokana na mazingira ya unyanyasaji wa kijinsia (West and Zondi-Mabizela 2004; West et al. 2004; West 2004). Wahusika husoma habari ya Tamari kwa uangalifu, wakitumia maswali yafuatayo: Nani wahusika wakuu, Je tunafahamu habari zao? Kila mhusika wa kiume amejihusisha na jambo gani katika kisa hiki cha ubakaji cha Tamari?; na Tamari anasema nini, na anafanya nini? Washiriki hutumia zana za wataalamu wa Biblia (km. zana za lugha ya Biblia). Kwa kufanya hivi, washiriki huchambua kifungu kwa undani zaidi kuliko kawaida yao. Baada ya uchambuzi huu, na kushirikishana ufahamu wao wa maandiko, basi washiriki hujadili maana ya kifungu hiki katika maisha yao halisi – yaani uzoefu wao wa maisha, wakitumia maswali haya: Je, wapo wanawake kama Tamari katika kanisa na jamii yako? Tusimulie habari zao. Je kuna theologia ya wanawake waliyowahi kubakwa au kunyanyaswa kijinsia? Je kuna zana, yaani mafundisho, ushauri, maelekezo, katika kanisa lako kwa ajili ya wahanga wa ubakaji?

Maswali yanayohusu kifungu cha Biblia na mazingira yetu yanawawezesha washiriki kugundua uhusiano wa theologia ya maisha ya jamii yao na Biblia. Kwa kuwa Biblia ni maandiko matakatifu, na maisha ya Wakristo yamejengwa katika msingi huu, basi washiriki hupata nguvu kwa njia ya kufahamu uhusiano wa maisha yao na maandiko ya Biblia, hasa zana za utaalamu wa Biblia zinapotumika huwezesha vifungu visivyozoeleka (kama vile 2 Samweli 13) visomwe, na vifungu vilivyozoeleka husoma kwa namna isiyozoeleka (tazama Mada ya 3). Kwa njia hii, wanawake ambao wamewahi kubakwa wanagundua kuwa hawako peke yao. Pia wanagundua kuwa licha ya kwamba kifungu cha Bibia kinahusiana na maisha yao, pia wanagundua kuwa wako wanawake wengine katika Mtaala wa Biblia ambao nao wana historia kama yao. Kwa hiyo theologia za maisha halisia zinapata nafasi ya kusikika.

Mtaala wa Biblia hauishii hapo tu. Swali la mwisho linalobaki ni hili: Utafanya nini kutokana na Mtaala huu wa Biblia? Vikundi vya Mtaala huweka mipangokazi mbalimbali itakayoshughulika na mifumo ya jamii; mara nyingi vikundi huweka mipangokazi itakayofikisha matokeo ya Mtaala wa Biblia ndani ya kanisa, ama kwa njia ya nyimbo, tamthilia, liturgia maalumu au kuanzisha kituo cha ushauri katika jamii au kanisani kwa ajili ya wahanga wa ubakaji. Wengine huanzisha njia mbalimbali za uelimishaji wa jamii au kanisa. Hizi ni njia mbalimbali za kurasimisha theologia ya maisha ya jamii baada ya jamii yenyewe kuieleza na kuimiliki.

Mada ya 2: VVU na UKIMWI

Watu wasioishi na VVU hujiuliza kwa nini wenye VVU wasome kufungu cha Mtaala wa Biblia kinachohusu ukoma? Kituo cha Ujamaa hufanya kazi na mtandao wa vikundi vya Siyaphila – ni vikundi vya wenye VVU na UKIMWI – na kupitia vikundi hivi tumejifunza kuwa washiriki huchagua vifungu ambavyo Yesu anaonyesha upendeleo wa dhati kwa wahanga wa unyanyapaa na ubaguzi wenye misingi ya kidini, na anapinga mifumo ya kibaguzi ya kidini na kijamii (West 2003). Kwa kuwa katika mazingira ya kawaida habari inayohubiriwa makanisani siyo habari njema kwa waathirika, basi matumaini yao ni kwamba katika maandiko kuna ujumbe zaidi ya ule unaohubiriwa. Hakika uzoefu na theologia ya maisha yao inathibitisha kuwa Mungu yupo pamoja nao. Hivyo huona injili inayobubiriwa makanisani siyo injili kamili ya Yesu, na kwa hiyo huigeukia Biblia kwa imani na hakika kuwa watasikia habari njema ya Yesu Kristo.

Waathirika huchagua vifungu ambavyo vina habari njema iliyo wazi zaidi; vifingu ambavyo Yesu anapinga kwa dhahiri mitazamo hasi ya jamii na theologia kandamizi, na anawaunga mkono wanaobaguliwa. Vifungu wanavyochagua vinathibitisha ufahamu wao wa uwepo wa Mungu kati yao. Hakika, pamoja na kushambuliwa na kanisa mara kwa mara, wanawake na wanaume wa Siyaphila wamesimama imara katika imani yao kuwa Mungu yupo pamoja nao. Theologia inayotokana na uzoefu wa maisha yao inawathibitishia kuwa Mungu yuko upande wao.

Hata hivyo, kama Mtaala wa Biblia kuhusu dhoruba baharini katika Marko 4:35-41 ulivyoeleza, ingawa Yesu yupo pamoja nao dhidi ya theologia kandamizi za kanisa, ziko nyakati wanapita katika dhoruba na kuhisi Yesu amelala. Wanasema wakati wa dhoruba “ni wakati wa kumuamsha Yesu! Hii ni theologia ya dhati kabisa kuhusu uwepo na ukimya wa Mungu katika mazingira ya VVU na UKIMWI! Wanatamani kanisa lingewasikia nyakati za ukimya.

Katika mtaala mwingine wa Biblia tuliyofanya na kikundi cha Siyaphila tulisoma kitabu cha Ayubu na kuchunguza kwa kina kuliko wafanyavyo katika makanisa yao. Katika kila shughuli ya mazishi, siku hadi siku wanakabiliana na maneno ya Ayubu: “Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana libarikiwe” (1:21); tuliamua kufafanua kwa pamoja sehemu za kitabu cha Ayubu ambazo hazisomwi kanisani. Tulisoma Ayubu sura ya 3 (West na Zengele 2004).

Sote tunajua Ayubu anakubali “mabaya” toka kwa Mungu, na anakaa kimya ili asitende dhambi kwa midomo yake (2:10) kwa kumhoji Mungu au theologia iliyopo. Akiwa amekaa kimya, marafiki zake wanakuja kumfariji (2:11). Tunajua marafiki watasema nini; kila mmoja anaeleza kuwa lazima Ayubu amefanya dhambi, hakuna namna nyingine ya kueleza sababu ya mateso yake. Kwa kuwa Ayubu ameshikwa na maradhi na ameisha, wanaona kuwa anaadhibiwa na Mungu kwa jambo fulani alilolifanya – hivi ndivyo theologia yao ilivyo (na ndivyo ilivyo theologia ya watu wengi siku hizi kuhusu VVU na UKIMWI – na hata Tsunami).

Kabla marafiki hawajasema jambo lolote, na kutoa ‘ushauri’, Ayubu anaongea. Hatimaye anapokea ushauri wa mke wake! Labda hofu ya kifo na kuangamia vilimnyamazisha. Hata hivyo, sasa changamoto ya mkewe imemuingia akilini. Katika nyaraka za asili za maandiko ya Mazoretiki kifungu hiki “Mkufuru [Mbariki] Mungu, ukafe” (1:10) kina maana kubwa kitheologia. Yaani kwa kuwa mwenye haki na kumbariki Mungu kunaleta shida kubwa kiasi

hiki, basi ni madhara gani yanaweza kutokea kwa kumkufuru Mungu? Baada ya kukataa "kufanya dhambi kwa midomo yake" hapo mwanzoni, sasa ameamua liwalo na liwe! Anaonekana kusita kufuata theologia ya mkewe kwa dhahiri, lakini Ayubu anamkufuru Mungu kwa namna fulani, kwa "kuilaani siku yake" ya kuzaliwa (3:1). Masimulizi hayatoshi kueleza kile Ayubu atakachosema, hivyo mashairi yanatumika. Mabadiliko haya ya mtindo wa maelezo ni ya kitheologia pia!

Huu ndiyo mwanza wa theologia nyingine; ni kilio cha ghadhabu na maumivu; ni mapambazuko ya theologia mpya. Analaani alichokifanya Mungu katika Mwanzo 1! Mungu anasema "na iwe nuru" (Mwanzo 1:3); Ayubu anapinga na kusema, "na iwe giza!" (kwa maelezo zaidi tazama Clines 1989:67-105); na Gutierez 1991:7-10). Ayubu anahangaika namna ya kumuelezea Mungu – namna ya kueleza theologia – katika mazingira magumu ya mateso na kufiwa. Je vifungu hivi visingefaa kusomwa katika mazishi mengi tunayoyafanya ya wenzetu ambao wamekufa kwa maradhi yatokanayo na UKIMWI. Je isingefaa tusome Ayubu 3:3-26 badala ya Ayubu 1:21: "Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana libarikiwe."

Tulisoma Ayubu 3 katika Mtaala wa Biblia na vikundi vya Siyaphila na tukaibua theologia ya maisha halisia ya hasira, maumivu, kukataliwa, upweke na kukatatamaa. Tulijifunza mengi kiasi kwamba theologia hii ya maisha halisia ilileta uponyaji na matumaini (West na Zengele 2004). Tulihitimisha kwa kumuomba kila mmoja aandike kilio chake binafsi kwa Mungu kwa kuzingatia Ayubu 3. Tumeyakusanya maelezo haya ya vilio kwa Mungu na tunakusudia kuyakabidhi katika makanisa ili wayatumie kwenye liturgia zao ili kuleta utajiri wa maisha ya kiroho.

Mada ya 3: Ardhi na uhakika wa chakula

Mada ya mwisho ni mfano wa mchakato wa mtaala wa Biblia unaotokana na kazi ya Ujamaa kuhusu Kanisa na Ardhi. Watumishi wa Kituo cha Ujamaa wamekuwa wakiendesha mfululizo wa mitaala ya Biblia kuhusu maswala ya ardhi Afrika Kusini. Ardhi na uhakika wa chakula ni moja ya maswala mtambuka ambayo watumishi wa Ujamaa wameombwa kuyajadili katika mitaala.

Baada ya kuwaza sana kuhusu vifungu vya kutumia kwa mtaala wa aina hii, mmoja wa washiriki katika maandalizi ya mtaala alishauri tutumie Sala ya Bwana. Wote tulikubaliana na hasa mshiriki huyo aliponukuu maneno haya, "Utupe leo riziki yetu". Ama kwa hakika maneno haya yanahusu uhakika wa chakula. Wengi wetu hatujawahi kuwaza kuwa kifungu hiki kinahusu uhakika wa chakula. Mhusika alipendekeza kifungu hiki kutokana na uzoefu wake wa maisha halisia katika mihangaiko yake ya uhitaji wa chakula cha kila siku. Wanakikundi cha jamii cha Ilimo, eneo la Amawoti karibu na Durban, walikiri wazi kwamba sentensi hii "Utupe leo riziki yetu" ina maana ya uhitaji wa chakula halisi kwa siku husika, na wala siyo methali fulani ya tabaka la walioshiba.

Basi katika mtaala huu washiriki waliweka mpangokazi utakaowezesha jamii yao kuwa na uhakika wa chakula cha kila siku: "Utupe leo riziki yetu" (Mathayo 6:11). Katika kifungu hiki Yesu anaiona jamii ambayo haina uhakika wa chakula, na anajua habari njema ya Mungu ni kwamba kila mtu awe na chakula cha kila siku. Mistari inayofuata ni mwendelezo wa ombi la

utupe leo riziki yetu. Maneno haya “Utusamehe deni zetu”, yasomwe katika mazingira ya uhakika wa chakuala na kuchunguza sababu za kutokuwa na uhakika wa chakula. Yesu anaonyesha sababu ya kutokuwa na uhakika wa chakula ni madeni ambayo tena yamesababisha wasiwe na ardhi – tatizo hili lilikuwa kubwa wakati wa Yesu. Wakati wa falme za Israeli, na baadaye wakati wa utawala chini ya viongozi wa hekalu, mara nyingi wakulima wadogo walikuwa wahanga wa madeni sugu (tazama Gottwald 1979, 1985; Pixley 1991). Yesu anafundisha kupitia sala kwamba kuwa na uhakika wa chakula siyo tu kuwa na chakula cha siku, bali pia kuwa na ardhi.

Hata hivyo, ili jamaii ya ufalme wa Mungu iwe yenye haki lazima wote wamfuatao Mungu siyo tu wasamehewe madeni yao, na kurudishiwa ardhi, bali pia wawasamehe wadeni wao, kama unavyosema mstari unaofuata katika sala hii: “kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu”. Matumizi ya lugha yanaashiria kuwa jamii inayoomba kusamehewa madeni imeshasamehe wadeni wake tayari, na sasa inamlilia Mungu kusamehe madeni yake. Kuwasamehe wengine madeni siyo jambo rahisi, kwa hiyo Yesu anawasihi waombe “Na usitutie majaribuni”, maana wanaweza kujaribiwa kutowasamehe wengine ili waendelee kunufaika kwa wadeni wao. Yesu anahitimisha sala yake kwamba Mungu “utuokoe [awaokoe wanyonge] na yule mwovu” (13). Ili kuwe na uhakika wa chakula lazima hatimaye tukombolewe toka katika uovu wa mifumo inayowafanya watu wawe wadeni.

Mawazo haya yalitokana na kikundi cha maandalizi ya mtaala wa Biblia kuhusu ardhi na uhakika wa chakula, na yakawa mbegu ya mtaala kwa kutumia Sala ya Bwana. Vikao vilivyofuata vilijengwa katika msingi huu.

Basi mada hii ya 3 ni kielelezo kuonyesha ushirikishaji wa zana na vitendeakazi vya utaalamu wa Biblia katika kukuza Mtaala wa Biblia wa Mazingira Halisia. Utaalamu wa maandiko namna hii unawasaidia washiriki wa mtaala hususani wanaharakati katika jamii; na kwa kutumia ufahamu na uzoefu wao, utaalamu wa maandiko unawaongezea utajiri katika kueleza, kumiliki na kurasimisha theologia zao za maisha halisia ya jamii.

Mada hii ina uwezo mkubwa wa kurasimisha theologia ya jamii kuhusu ardhi na uhakika wa chakula, kwa kuwa tukiomba sala hii tukiwa na mtazamo huu katika makanisa yetu, tunashiriki kwa vitendo kutengeneza njia kwa ajili ya mfumo wenye haki zaidi wa kijamii na kiuchumi.

Hitimisho

Katika msingi wa theologia ‘rasmi’ ya umma tuliyoizoea, ipo theologia ambayo inaibuka ingawa haijadhihirika. Theologia hii inatokana na imani tunayoiishi na uzoefu wa maisha, theologia hii inachipua na haijakamilika bado. Ni changamoto kwa kanisa, kwamba linapaswa kuikumbatia theologia hii ili ikubalike na umma wote wa kanisa. Ni kwa njia hii tu ndipo kanisa litakuwa nyumba na mahali salama kwa wanawake, watu waishio na VVU na UKIMWI, waliosahaulika na kunyanyaswa na jamii, na maskini.

Marejeo

Brueggemann, Walter. 1993. Trajectories in Old Testament literature and the sociology of ancient Israel. In The Bible and liberation: political and social hermeneutics, edited by N. K. Gottwald and R. A. Horsley. Maryknoll, NY: Orbis.

Clines, David J.A. 1989. Job 1-20. Dallas: Word Books.

Cochrane, James R. 1999. Circles of diginity: community wisdom and theological reflection. Minneapolis: Fortress.

———. 2001. Questioning contextual theology. In Towards an agenda for contextual theology: essays in honour of Albert Nolan, edited by M. T. Speckman and L. T. Kaufmann. Pietermaritzburg: Cluster Publications.

Dumortier, J.M. 1983. Many in this city are my people: Young Christian Workers. Durban: Young Christian Workers.

Gottwald, Norman K. 1979. The tribes of Yahweh: a sociology of the religion of liberated Israel, 1250-1050 B.C. Maryknoll, New York: Orbis.

———. 1985. The Hebrew Bible: a socio-literary introduction. Philadelphia: Fortress.

Gutierrez, Gustavo. 1991. On Job: God-talk and the suffering of the innocent. Maryknoll, NY: Orbis Books.

Haddad, Beverley G. 2000. African women's theologies of survival: intersecting faith, feminisms, and development. PhD, School of Theology, University of Natal, Pietermaritzburg.

Mesters, C. 1984. The use of the Bible in Christian communities of the common people. In The Bible and liberation: political and social hermeneutics, edited by N. K. Gottwald and R. A. Horsley. Maryknoll, NY: Orbis Books.

Mesters, Carlos. 1989. Defenseless flower: a new reading of the Bible. Translated by F. McDonagh. Maryknoll, NY: Orbis Books.

Nadar, Sarojini. 2003. Power, ideology and interpretation/s: womanist and literary perspectives on the book of Esther as resources for gender-social transformation, School of Theology, University of Natal, Pietermaritzburg.

Nolan, Albert. 1996. Work, the Bible, workers, and theologians: elements of a workers' theology. Semeia 73:213-220.

Perdue, L. G. 1991. Wisdom in revolt: metaphorical theology in the book of Job. Sheffield: Almond Press.

Philpott, Graham. 1993. Jesus is tricky and God is undemocratic: the kin-dom of God in Amawoti. Pietermaritzburg: Cluster Publications.

Pixley, George V. 1991. A Latin American perspective: the option for the poor in the Old Testament. In Voices from the margin: interpreting the Bible in the Third World, edited by R. S. Sugirtharajah. Maryknoll, NY: Orbis.

Scott, James C. 1990. Domination and the arts of resistance: hidden transcripts. New Haven and London: Yale University Press.

Society, The Scottish Bible, and The Contextual Mtaala wa Biblia wa Group. 2005. Conversations: the companion. Glasgow: Scottish Bible Society.

Speckman, McGlory T., and Larry T. Kaufmann. 2001. Introduction. In Towards an agenda for contextual theology: essays in honour of Albert Nolan, edited by M. T. Speckman and L. T. Kaufmann. Pietermaritzburg: Cluster Publications.

Stevens, I.D. 1985. The role of the church in industry and industrial relations; focusing on the supportive role with worker organisations, especially the independent trade unions in South Africa. Honours, University of Natal, Pietermartizburg.

theologians, Kairos. 1986. The Kairos document: challenge to the church. Revised Second Edition ed. Braamfontein: Skotaville.

Villa-Vicencio, Charles. 1989. Right wing religion: have the chickens come home to roost? Journal of Theology for Southern Africa 69:7-16.

West, Gerald O. 1995. Biblical hermeneutics of liberation: modes of reading the Bible in the South African context. Second Edition ed. Maryknoll, NY and Pietermaritzburg: Orbis Books and Cluster Publications.

———. 2003. The academy of the poor: towards a dialogical reading of the Bible. Pietermaritzburg: Cluster Publications. Original edition, Sheffield Academic Press, 1999.

———. 2003. Reading the Bible in the light of HIV/AIDS in South Africa. The Ecumenical Review 55 (4):335-344.

———. 2004. 1 and 2 Samuel. In Global Bible commentary, edited by D. Patte. Nashville: Abingdon Press.

West, Gerald O., and Bongi Zengele. 2004. Reading Job ‘positively' in the context of HIV/AIDS in South Africa. Concilium 4:112-124.

West, Gerald O., and Phumzile Zondi-Mabizela. 2004. The Bible story that became a campaign: the Tamar Campaign in South Africa (and beyond). Ministerial Formation 103:4-12.

West, Gerald O., Phumzile Zondi-Mabizela, Martin Maluleke, Happiness Khumalo, P. Smadz Matsepe, and Mirolyn Naidoo. 2004. Rape in the house of David: the biblical story of Tamar as a resource for transformation. Agenda 61:36-41.